# Pambazuko

Toleo Namba 155 | Jumatatu, Februari 16-22, 2026

# Asilimia 30 ununuzi wa umma bado kizungumkuti

- Ni kuhusu makundi maalum

Uk. 6&7

## Wizi washamiri katika hospitali za serikali Uk. 15



Dkt. Mwinyi

# Mwafaka SUK Zanzibar wanukia

Habari Uk. 16 &17



Othman

**Jicho la Tai**

## Waziri Gwajima acha nywila ya mume wako

JUZI nikiwa nimejilaza sebuleni baada ya kumeza dawa zangu za presha, huku nikiperuzi mitandao ya kijamii, nakutana na klipu moja yenye sauti ya mtu ninayemkubali sana.

Safu Uk. 5



Uk. 12

# Lissu ashangaza

## Tahariri

# Pongezi Siku 100 sawa, lakini bado

KATIKA siku 100 tangu kuingia Ikulu, Rais Samia Suluhu Hassan amethibitisha kuwa ahadi zake za kampeni hazikuwa maneno tu bali vitendo vinavyoonekana.

Miradi ya maendeleo ya msingi, uimarishaji wa huduma za afya na elimu, pamoja na sera za kuhimiza uwekezaji zimepata msukumo mpya, huku baadhi zikitimizwa.

Uamuzi wa kuharakisha utekelezaji wa miradi ya miundombinu na kuboresha mazingira ya biashara umekuwa chanzo cha matumaini kwa wananchi wengi waliokuwa wakisubiri mabadiliko.

Hii ni hatua inayostahili pongezi, kwani inaonyesha uelewa wa kuhudumia wananchi na kuleta matokeo ndani ya muda mfupi – wa siku 100 kama alivyoahidi.

Hata hivyo, Pambazuko tunaeleza kuwa mafanikio haya hayapaswi kutufanya tupuuze changamoto kubwa zinazowakabili Watanzania; rushwa, matumizi mabaya ya fedha za umma, na ukandamizaji wa baadhi ya haki za msingi kunakofanywa na baadhi ya watendaji wa serikali, hasa vyombo vya usalama, na hasa Jeshi la Polisi.

Kushangilia kutimizwa kwa ahadi na hata kwa maendeleo yaliyofikiwa, kunapaswa kutoa msukumo mpya na wenye nguvu kuhakikisha uwajibikaji, uwazi na haki kwa wote vinatendeka na kuchukuliwa kwa hatua kali kwa watendaji wanaokiuka tunu hizo.

Serikali inatakiwa kuonyesha dhamira thabiti ya kuziba mianya ya rushwa kwa kuimarisha taasisi za ukaguzi, kuendesha uchunguzi huru na kusimamia sheria kwa wote bila upendeleo. Huku wananchi nao tukiwahimiza kuichukia rushwa na uzembe.

Matumizi mabaya ya fedha za umma ni tishio ambalo linaweza kuinyima taifa fursa ya kuendeleza miradi ya maendeleo. Ni muhimu serikali iwe na mfumo madhubuti wa ununuzi, uwiano wazi wa matumizi, na ushiriki wa jamii katika ukaguzi wa miradi.

Aidha, heshima kwa haki za binadamu na uhuru wa kujieleza ni nguzo muhimu za demokrasia zinazofaa kwa maendeleo endelevu, kwa Watanzania wote.

Serikali inapaswa kuhakikisha kwamba hatua za kisheria na kiusalama hazitumiwi kuwakandamiza, na pengine hata kuwaonea wale wenye fikra tofauti za kisiasa na hata wanaokwenda kinyume na misimamo ya viongozi wa serikali.

Mazungumzo ya namna ya kupata muafaka endelevu wa Tanzania, yenye uwazi na shirikishi kwa wadau mbalimbali; katika siasa, kijamii na kibiashara, yatasaidia kujenga imani na kupata suluhu za pamoja.

Rais Samia ametoa mfano mzuri wa kuwaweka wananchi mbele kupitia utekelezaji wa ahadi. Sasa ni kipindi cha kuimarisha mifumo inayolinda nafasi za umma, kuweka uwazi, na kuheshimu haki za raia. Kwa kufanya hivyo, nchi itaendelea kuona manufaa ya sasa na kuhakikisha kuwa maendeleo yanadumu.

Serikali, vyombo vya sheria, vyama vya kiraia na wananchi wote wanapaswa kushirikiana kutengeneza Tanzania yenye uwazi, haki na ustawi kwa vizazi vya sasa na hata vijavyo.

Tuikubali, tuitunze na kuistawisha Tanzania yetu kwa pamoja.

## Go Green yazinduliwa...




*Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, Dkt. Kedmon Mapana (kulia) akiwasikiliza mabalozi CRDB Foundation- iMbeju wakati wa uzinduzi wa Program ya Go Green uliofanyika jijini Dodoma wiki iliyopita. (Picha na Mpigapicha Wetu).*

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**


## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mhariri wa Habari** | : | Maregesi **PAUL** | 0689 732 325 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

# Dunia: Hapa na pale

## Ukraine yadungua Russia

MASHAMBULIZI ya droni ya Ukraine yameharibu ghala kubwa la mafuta katika eneo la kusini la Krasnodar, nchini Russia.

Taarifa ya maofisa wa usalama wa Russia iliyotangazwa jana inaeleza kuwa Ukraine inaendelea kulenga hifadhi za mafuta za Russia ikiwa ni kisasi baada ya nchi hiyo ya Russia kuua maelfu ya Waukraine.



Eneo hilo lililoshambuliwa ni maarufu kwa kuwa na hifadhi kubwa ya mafuta na chakula, hasa ngano. Hali ni mbaya zaidi kwani matenki ya mafuta na hifadhi nyingine za vyakula zimeharibiwa vibaya.

Ofisa mmoja amesema kuwa katika mashambulizi hayo, watu wawili walijeruhiwa wakati wa shambulio hilo.

Wizara ya Ulinzi ya Russia imeeleza kuwa imefanikiwa kutungua droni 88 za Ukraine katika mipaka ya kusini mwa nchi.

## Afungwa akidhulumu maiti

MMILIKI mwenza wa mochwari katika Jimbo la Colorado, Marekani amehukumiwa kifungo cha miaka 40 gerezani baada ya kupatikana na hatia ya kudhulumu maiti karibu 200.

Inaelezwa kuwa mmiliki huyo aliacha kuchoma miili hiyo, na badala yake aliwapa ndugu zao majivu bandia baada ya kuwalaghai kwamba miili imechomwa na kwamba majibu anayowapa ndugu yanayotokana na mabaki ya ndugu zao.

Kabla ya hukumu kutolewa, Jon Hallford aliomba msamaha mahakamani na kusikiliza familia za waathiriwa zikisimulia jinsi wanavyosumbuliwa na ndoto mbaya wakiwazuia wapendwa wao "wakiharibika" chini ya uangalizi wake. Mke wake anakabiliwa na kesi hiyohiyo.

## Vijana wafurahia ubunge

BANGLADESH bado imo katika furaha baada ya wananchi wengi kupiga kura kwa wingi kuwezesha ushindi wa wabunge wengi vijana katika uchaguzi uliofanyika Alhamisi iliyopita - Februari 12, 2026.

Ushindi huo unatarajiwa kuleta udhabiti katika nchi hiyo ambayo ilikuwa imeathiriwa vibaya na wimbi la maandamano yasiyokuwa na kikomo yaliyotawala kwa kupigania uongozi bora mnamo 2024.

Uchaguzi huo wa kwanza kuandaliwa tangu Gen Z washiriki maandamano 2024 yaliyomwondoa madarakani aliyekuwa Waziri Mkuu Sheikh Hasina.

Maandamano hayo ambayo yalisababisha vifo vya vijana wengi yalivuruga uchumi wa taifa hilo na kusababisha viwanda viporomoke. Vijana wengi waliuawa na maofisa wa usalama wakati wa maandamano hayo.

## Ethiopia sasa yabambwa

SASA imebainika kuwa Ethiopia inaendelea kuwa eneo la siri la mafunzo ya kijeshi kwa wapiganaji wa RSF katika taifa jirani la Sudan.

Taarifa za siri ambazo zimepatikana kwa umma zinaeleza kuwa uwepo wa kambi hiyo unaonyesha kwamba Ethiopia inahusika moja kwa moja na ghasia za kijamii ambazo zinaendelea kati ya wanajeshi wa serikali na wapiganaji wa RSF Sudan.

Duru kadhaa kutoka Serikali ya Ethiopia zilisema kuwa kambi hiyo ya kijeshi inadhaminiwa na baadhi ya wanachama wa Umoja wa Nchi za Kiarabu (UAE). Umoja huo umekuwa ukikanusha kuhusika.

Vita vya kijamii Sudan vilianza mnamo 2023 kati ya wanajeshi wa Sudan na RSF kuelekea mchakato wa kukabidhi utawala wa taifa hilo kwa raia.

Na Mzee TAI

# Waziri Gwajima acha nywila ya mumeo

JUZI nikiwa nimejilaza sebuleni baada ya kumeza dawa zangu za presha, huku nikiperuzi mitandao ya kijamii, nakutana na klipu moja yenye sauti ya mtu ninayemkubali sana.

Awali nilidhani masikio yangu yamepoteza uwezo wa kusikia vizuri kama ambavyo maozi yangu yanavyopata changamoto kuona.

Nikaamua kukaa kitako na kuitisha miwani yangu. Nilitaka kujiridhisha kama hicho nachosikia kinatoka kwa binti yangu, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima (pichani).

Sikutaka kuamini mapema kwa kuwa matamshi yale yalinipa jakamoyo; kwamba Waziri Gwajima chukua, hupekua na wakati mwingine kujitumia fedha kutoka kwenye simu ya mume wake.

Haraka-haraka nikatafuta namba yake kwenye simu, nikaikosa, nikaitisha kwa kijana wangu ninayeamini anayo, Kumbe naye hana. Basi, nikaishia kukasirika.

Hakika kauli yake ilinishtua sana, maana ni jana tu nilikuwa nasuluhisha ugomvi wa binti wa mdogo wangu ambaye amevurugana na mumewe kwa kuwa alishika, akapekua na kusoma baadhi ya ujumbe ambao ni binafsi wa mume wake.

Ugomvi huo haukuwa wa kwanza kusuluhisha, bali kila mara nakuwa mtu wa kati kutafuta suluhu baada ya mume na mke kuvurugana sababu kubwa ikiwa ni "kushikiana simu."

Katika kuamua vurugu hizo, ushauri wangu mkubwa ni kuwakanya kuchukua, kupekua na kujitumia iwe fedha ama ujumbe binafsi kwenye simu.

Kiasi fulani ushauri huo umesaidia, kwani idadi ya wanaokuja kuchukua busara zangu na kusuluhisha wanandoa kuhusu kupekua simu ya mwenzi, inapungua.

Lakini sasa, kwa kauli ya Waziri Gwajima ni kwamba huenda ikachochea upekuzi wa simu za wenza na hapo naona nikitenga muda wangu mwingi kuendelea kusuluhisha.

Ninashangaa iweje Waziri Dorothy Gwajima, hata kama wanapendana kiasi gani na



mume wake auambie umma – kupitia televisheni kwamba huchukua, hufungua, hupekua na kujitumia picha na hata fedha kutoka kwenye simu ya mwenza wake?

Hivi Waziri Gwajima ananitaka mimi nini. Yaani nianze tena kusuluhisha wanandoa kwa kuwa wanapekua simu za mwenza. Kama wanapendana sana kiasi cha kupeana hadi nywila, kwanini aseme kwa televisheni?

Haoni kwamba sasa anawapa kiburi wanandoa kuanza kuvunja mipaka ya kupekuliana simu za mkononi ambazo, kimsingi ni binafsi mno!

Waziri Gwajima haoni kwamba sasa anapeleka ujumbe kwamba wanandoa waepuke mipaka na kuvunja umimi wa simu binafsi. Yaani anataka faragha zivunje kabisa.

Mimi na uzee wangu nimeona mengi, hata kama wapo wasiokuja kwangu kupata busara zangu, lakini nina uhakika kuwa wanandoa wanaogombana sababu kubwa ni matumizi ya simu na kuingilia faragha.

Kutokana na hilo, sasa namuomba Waziri Gwajima ajitokeze tena kwenye televisheni na kutamka kwamba alikuwa anatania tu, vinginevyo akikaa kimya, huko kwenye familia, kuna moto utaanza kuwaka kwa kuwa wengi wataamini ni haki na wajibu wenza kugawana nywila na pengine hiyo ni ruksa ya kitaifa kwa kila wanandoa.

Habari Kuu

# Asilimia 30 ununuzi wa umma bado kizungumkuti



Na Elizabeth HOMBO

PAMOJA na serikali kueleza kuwepo jitihada za kusambaza elimu juu ya ununuzi wa umma, imebainika watu wengi – ndani ya makundi maalum hawana ufahamu hata wa kuwepo zabuni hiyo.

"Ndiyo nasikia kwako kuhusu habari ya zabuni, mimi maisha yangu yote kazi yangu ni kupika na nasomesha watoto wangu peke yangu baada ya baba yao kukimbia majukumu," hiyo ni kauli ya Hadija Athumani (45), mama anayejishughulika na biashara ya kuuza chakula, maarufu kama mama ntilie.

Hadija, ambaye hufanya biashara yake hiyo ya kuuza chakula katika eneo la stendi ya daladala ya Mbezi Luis, Dar es Salaam, alitoa kauli hiyo baada ya kuulizwa na gazeti hili kuhusu uelewa wake juu ya sheria ambayo imetenga asilimia 30 ya zabuni kwa ununuzi wa umma kwa makundi maalum.

Sheria ya Ununuzi wa Umma inaelekeza kuwa kila mamlaka ya ununuzi itenge asilimia 30 ya ununuzi unaofanyika kwa mwaka kwa ajili ya makundi maalum.

Hadija, kwa kazi anayoifanya, anaangukia katika makundi maalum, lakini hana habari kuhusiana na sheria hii inayotoa upendeleo kwake.

Kwa mshangao akaendelea kuhoji: "Sasa kama kuna jambo kama hilo kwa nini hatushirikishwi sisi wanawake tunaopambana peke yetu? Mbona wakati wa kampeni wanapita hapa wakiomba kupigiwa kura?"

Alisisitiza kuwa haelewi chochote kuhusu asilimia 30 ya ununuzi wa umma kwa makundi maalum wala kuhusu mfumo wa NeST – ambao ni mfumo wa ununuzi wa kielektroniki unaotumika kusajili watu na taasisi zinazoomba zabuni za serikali.

Hadija ni miongoni mwa wananchi walio wengi katika Halmashauri ya Ubungo, Dar es Salaam ambao hawana uelewa kuhusu asilimia 30 ya ununuzi wa umma kwa makundi maalum.

Swali la kujiuliza ni je, kama walio katika maeneo ya mjini hawana uelewa kuhusu upendeleo huu unaotolewa kisheria kwa makundi maalum, vipi kuhusu wale walio vijijini?

**Sheria inavyotaka**

Kifungu cha 73(1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya 2023, kinazitaka taasisi zote za umma kuhakikisha kuwa kazi za ununuzi, ugavi na uondoshaji mali zinafanywa na kutolewa taarifa kupitia mfumo wa kielektroniki wa manunuzi ya umma (NeST).

Kanuni ya 34(2) ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ya mwaka 2024, inatamka kuwa chombo kinachohusika na makundi maalum lazima kihakikishe kuwa mafunzo muhimu yanatolewa kwa vikundi hivyo kabla ya kupewa cheti cha usajili ili viweze kushiriki kwenye mchakato wa ununuzi wa umma.

Sheria hiyo ilitoa upendeleo kwa makundi hayo, kupata fursa ya kupata zabuni, kukuza biashara ndogo ndogo ili kupunguza ukosefu wa ajira.

Inaendelea Uk.7

# Asilimia 30 ununuzi...

Inatoka Uk. 6

**Mwongozo wa PPRA**

PPRA imeandaa mwongozo wa namna makundi maalum yanavyoweza kushiriki kwenye mchakato wa ununuzi wa umma kwa urahisi.

Maofisa wa PPRA waliozungumza na Pambazuko wanasema mwongozo huo umeandaliwa ili kuzisaidia taasisi za umma na wanachama wa makundi hayo, kuelewa taratibu na vigezo vya utekelezaji wa asilimia 30.

Mwongozo huo unaelekeza kuwa katika hizo asilimia 30, vijana wanapaswa kupata asilimia 10 ya zabuni zilizotengwa, watu wenye ulamavu asilimia 10, wanawake na wazee asilimia 5 kila Kundi.

Kwa mujibu wa mwongozo huo, kila taasisi inapaswa kuwa wazi kuhusiana na jambo hili.

**Mfumo wa NeST**

Ili kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji katika michakato ya ununuzi wa umma unaowezesha ushiriki mpana hasa kwa makundi maalum, serikali ilianzisha mfumo wa kidijitali wa NeST.

Hata hivyo, pamoja na uwepo wa sheria, kanuni, mwongozo na mfumo huu, bado watu wa makundi maalum maeneo mengi nchini, ikiwemo Manispaa ya Ubungo, hawana uelewa kuhusu sheria na NeST.

PPRA yenyewe imekiri kuwa pamoja na elimu kubwa wanayoendelea kuitoa kuhusiana na masuala hayo, lakini bado ushiriki wa makundi maalum ni mdogo.

Ripoti mbalimbali za masuala ya ununuzi wa umma, nazo zinabainisha changamoto nyingi zinazowakabili watumiaji wa mfumo wa NeST, hasa wale wa makundi maalum.

Wengi wanakabiliwa na kutojua matumizi ya teknolojia na vikwazo vya kiufundi katika kutumia mfumo huo.

**Ni asilimia mbili tu zilizotekelezwa**

Uchunguzi wa Pambazuko umebaini kuwa ni asilimia mbili tu ya thamani ya asilimia 30 ya ununuzi wa umma inayotengwa kwa ajili ya makundi maalum ndio hutumika kwa ajili ya makundi hayo.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Tanzania (Shivyawata), Jonas Lubago ameliambia gazeti hili kuwa jambo moja ambalo wanashukuru ni kwamba walishiriki kwenye uandaaji wa kanuni mpya ya mwaka 2024.

Hata hivyo, anasema inasikitisha sasa kuwa ushirikishwaji katika utekelezaji umepungua sana.

Anasema makundi ya walemavu yanakabiliwa na changamoto lukuki kushiriki kwenye mchakato wa ununuzi wa umma. Mathalani, anasema wanatakiwa kuwa na kampuni au vikundi viliyosajiliwa.

Kuhusu mafunzo ya NeST, anasema mafunzo hayo ni kweli yanatolewa lakini anahisi wanaopata mafunzo si wahusika na bado hatua haijachukuliwa kuhakikisha wahusika wanafikiwa na mafunzo hayo.

"Mafunzo tunapata lakini tunakosa tu pesa mfano Stanbic imeandaa mafunzo… sasa changamoto iliyopo watu hawana nauli na Stanbic wamesema sera yao hairuhusu kutoa nauli. Wengine ndio wanapambana," anasema Lubago.

Anaeleza kuwa changamoto nyingine ambayo wanakumbana nayo watu wa kundi lake ni ukosefu wa mtaji. Anasema ikitokea wakapata tenda hawana mtaji wa kuanzia na pia malipo ya serikali huwa yanachelewa.

"Sasa kama mtu nauli tu anakosa sasa mtaji atautoa wapi, jambo hili huwa inatukatisha tamaa wengine," anasema.

Katika hilo anapendekeza kuwa angalau uwekwe utaratibu wa kupata mikopo ya asilimia mbili ya halmashauri ili wanapopata tenda iwe rahisi kwao kutekeleza.

**Chemba ya wanawake**

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC), Mwajuma Hamza akizungumzia kuhusu endapo wamekuwa wakitoa elimu ya NeST kwa wanawake wajasiriamali, anasema mafunzo yote yamekuwa yakiandaliwa na PPRA na wao kualikwa.

Inaendelea Uk.8

# Asilimia 30 ununuzi...

Inatoka Uk. 7

“Hata ukihitaji data yoyote lazima uende PPRA ndio watakupa. Lakini kuhusu mafunzo wanawake huwa wanapata kupitia PPRA, inatuunganisha kwa pamoja hata ikitokea changamoto yoyote ni PPRA wamekuwa wakitusaidia kutoa elimu,” anasema Mwajuma.

Kwa upande mwingine, Meneja wa Uhusiano wa Veta, Sitta Peter, anasema wao hawahusiki na kutoa mafunzo kwa vijana kuhusu NeST, bali wahusika wakuu ni PPRA.

Anasema jambo ambalo wamekuwa wakilifanya ni kuwahamasisha wahitimu wanapomaliza wajisajili kwenye NeST ili waweze kupata tenda.

### PPRA wanena

Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa PPRA, Remija Salvatory, anasema wamekuwa wakitoa mafunzo kwa muda mrefu na bado wanazidi kuongeza nguvu ili elimu izidi kuwafikia watu wengi.

Kwa upande wake Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa PPRA, Joseph Muhozi anasema wamekuwa wakizunguka kote nchini hadi maeneo ya vijijini wakitoa elimu lakini bado wanaojiunga ni wachache.

“Tumekuwa tukizunguka mpaka vijijini tangu mwaka 2022 kutafuta watu wa kupata tenda maana kila halmashauri ina tenda za serikali.

“Hatufanyi tu mjini, tunazungumza na watu wa chini, na tukapata vikundi zaidi 1,200 nchi nzima. Lakini bado wengi hawana imani na hizi tenda hata wanaoamini baadhi yao pia wanapotosha wengine wanaogopa ushindani kwamba unapofungua fursa ushindani unakuwa mkubwa,” anasema.

Muhozi anasema tayari wametoa mafunzo kwa maofisa maendeleo ya jamii kila kwa halmashauri nchini pamoja na wakurugenzi wote nao wanaelewa kuhusu mfumo wa NeST.

### Tenda za bilioni 30 zimetolewa

Muhozi anasema tangu ulipoanza mfumo wa NeST hadi sasa zimetolewa tenda zenye thamani ya shilingi bilioni 30 kwa makundi maalum.

Anasema changamoto iliyopo ni pamoja na kuwepo fursa nyingi lakini watu ni wachache tu wanaojitokeza na kwamba wengine wanakuwa tayari wamejisajili kwenye mfumo wa NeST lakini hawaombi tenda zinapotangazwa.

Akizungumzia kuhusu uelewa mdogo wa mfumo wa NeST kwa makundi hayo kupata tenda, Muhozi anasema hakuna mfumo wa kielektroniki usiokuwa na changamoto.

“Unajua kabla huu mfumo ulipokuwa haujaanza tulishaufanyia majaribio baada ya kugundua kuna changamoto kadha wa kadha ndio maana tunatumia nguvu kubwa kutoa elimu,” anasema.

Alipoulizwa kuhusu bajeti ambazo wanatumia kutoa elimu, anasema hawawezi kusema moja kwa moja kwa sababu zingine wamekuwa wakifanya bure.

### Wengi hawaelewi

Kwa upande wake, kijana Joseph Shirima (33) anayefanya biashara ya vifaa vya umeme katika eneo la Shekilango, anasema aliwahi kusikia kuhusu asilimia 30 ya ununuzi wa umma kwenye redio lakini hakuelewa.

“Hiyo NeST sijui kwa kweli lakini kuhusu asilimia 30 ya ununuzi wa umma niliwahi kusikia kwenye redio lakini sikuwa najua kumbe hata sisi vijana tunapaswa kushiriki,” anasema. Naye Prossy Iddy (47), anayejishughulisha na biashara ya vinywaji vya jumla katika eneo la Sinza, anasema hafahamu kuhusu kujiandikisha kwenye NeST isipokuwa waliwahi kuunda kikundi chao na kuomba mkopo wa asilimia 2 lakini hawakupata.

“Ninachojua tuliwahi kuunda kikundi chetu tukaenda kuomba mkopo wa halmashauri lakini leo ni mwaka 4 hatujawahi kuitwa tena.

“Kuhusu hizo asilimia 30 kwa makundi maalum na kujisajiri kwenye hiyo NeST unayoisema hatujawahi kupewa elimu yoyote,” anasema Prossy.

January Khamis (35) mkazi wa Ubungo, ambaye ni fundi ujenzi anasema amewahi kusikia kuhusu NeST na bosi wake aliwahi kupata tenda ya kwenda kujenga nyumba za NSSF kule Arusha, lakini changamoto iliyopo mfumo huo una ugumu.

“Kwa mfano sisi mafundi wa kawaida kuutumia ni shida sana kuna kipindi tulishakosa zabuni ya ujenzi baada ya kukosea kujaza kwenye mfumo,” anasema.

Rashidi Hamis (33) fundi ujenzi katika eneo la Mbezi Luis, anasema aliwahi kusikia neno ununuzi wa umma lakini hakufuatilia.

Inaendelea Uk.9

# Asilimia 30 ununuzi...

Inatoka Uk. 8

“Sasa kama kuna jambo zuri kama hilo kwanini hawa viongozi wa mtaa wasiwe wanatupa elimu ili tuweze kushiriki au hizo tenda zinaenda kwa wapigaji ndio maana hawataki kutupa elimu,” alihoji Hamis.

**Diwani Sinza atupa mpira**

Diwani wa Kata ya Sinza, Raphael Awino, alipoulizwa endapo wamewahi kutoa elimu ya NeST kwa makundi maalum katika eneo lake, alimtaka mwandishi amtafute Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo kwa taarifa sahihi.

Hata alipotakiwa kuwa azungumzie yeye kama diwani kama aliwahi kutoa elimu kuhusu NeST katika eneo lake, bado alimtaka mwandishi wa habari hizi amtafute mkurugenzi.

“Suala la mahojiano si ni la hiari? Sasa unataka nikujibu ndiyo au hapana? Kwa taarifa sahihi naomba umtafute Mkurugenzi,” alisisitiza.

**Watendaji wa kata**

Mtendaji wa Mtaa wa Njeteni Kata ya Kwembe, Agness Kulebelwa anasema pamoja na kwamba amewahi kushiriki mafunzo kuhusu NeST lakini bado elimu inahitajika zaidi.

“Kwanza waboreshe upatikanaji wa mtandao, pamoja na kwamba nimewahi kushiriki mafunzo lakini bado ule mfumo una ugumu sasa kwa wananchi wa kawaida itakuwa ngumu zaidi,” anasema Agness.

**Urasimu Manispaa**

Kwa upande wake, Mtendaji wa Kata ya Ubungo aliyejitambulisha kwa jina moja la Elizabeth aligoma kutoa ushirikiano akisema hadi apate kibali kutoka kwa Mkurugenzi.

January 22, 2025, alipotafutwa Ofisa Habari wa Halmashauri ya Ubungo, Joina Nzali ili kupata miadi ya kukutana na mkurugenzi pamoja na maofisa wengine, alimtaka mwandishi kuwasiliana na Said Sindo kwa kuwa yeye hakuwa ofisini.

“Salama tu za kwako, okay sawa kwa sasa sipo ofisini wasiliana na Said Sindo atakupa ushirikiano,” alisema.

Baada ya mwandishi kumtafuta Sindo aliahidi angerumdia lakini hakufanya hivyo.

Alipotafutwa tena ndipo akamjibu mwandishi kwa ujumbe mfupi wa maneno kuwa: “Unajua kuna wakuu wa idara hawawezi kuongea kama hawajapewa maelekezo na mkurugenzi ndiye msemaji wa taasisi…”

“Kwa hiyo namaanisha utume barua ya kumuomba Mkurugenzi juu hicho unachokihitaji. Utatuma kwa email; md@ubungomc.go.tz,” aliandika Sindo.

Baada ya mwandishi kufanya hivyo na kutuma barua hiyo, baadaye alimtaka tena kuambatanisha barua pamoja na maswali.

Baada ya mwandishi kufanya hivyo, mara kadhaa alikuwa akimtaka mwandishi kuwa atamrudia.

Februari 3,2025, alimtaka mwandishi amtafute tena Joina.

“Mtafute Joina amesharudi, aliniambia atafuatilia kuhusu hiyo email,” alisema Sindo.

Alipotafutwa Joina alimtumia barua mwandishi kuwa ombi limekubaliwa na anatakiwa afike ofisi ya mkurugenzi Februari 16, 2025 kwa ajili ya mahojiano.




***Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba (kulia), akisalimiana na wananchi wa Kilindi mkoani Tanga baada ya kukagua mradi wa maji wa Kwamaligwa uliopo wilayani humo ambao utagharimu kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni 6 hadi kukamilika. Alikuwa na ziara wilayani humo juzi. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).***



Na Dkt. Benson BAGONZA

# Ikibaki siri tutanufaika wote



SIKU moja akaja mke wa "Mjaluo" mmoja aliyekuwa waziri. Kaniomba nimuombee mumewe ambaye ni waziri na ni "Mjaluo." Baada ya sala, akaleta la pili.

Akasema watoto wao wanapata shida kumwona baba yao kwani anatukanwa mbele ya televisheni. Imefika mahali wanaogopa kuifungua kwa kuhofia watakuta baba yao anatukanwa na boss wake.

Nikamjibu, "boss wa mumeo, ndiye boss wa taifa japo sisi huwa ni maboss wake wakati wa uchaguzi." Nikamuahidi kuwa siku nikikutana naye nitamwambia. Ningeshauri;

Kwamba boss ana uhuru wa kuteua na kutengua. Asitokee anayehoji mpaka tubadili mkataba.

Kwamba sababu za kuteua na kutengua, zingebaki siri ya mteuaji. Kumsifia mtu wakati anateuliwa halafu "akabwatukiwa" wakati anatenguliwa, inauguza wengi wakiwamo watoto, michepuko mpaka wapishi wa nyumbani.

Kwamba sifa kemkem wakati wa uteuzi zikifuatwa na kimya wakati wa kutenguliwa, nako ni shida. Bora kote kuwe kimya.

Kwamba Watanzania hatuna dogo. Akisema, tunazua. Asiposema, tunabuni, lakini bora kimya. Na kiwe kimya kweli hata kwa washauri na machawa. Tukumbuke, kuna watu wanalizwa pochi zao ili wateuliwe! Hakuna risiti, msinifuate kama Shabiby.

Kwamba kuna aliyeanzisha huu utamaduni wa kusema kwa nini. Natamani uachwe. Sema tu, dira yetu inadai mabadiliko. Itatosha na kubaki.

Ukichokonoa sababu, kuna watu watanyimwa unyumba. Walidhaniwa wa maana kumbe wa ovyo tu. Kambarage alikuwa haongei siku ya kuapisha watu "uwongo". Alipolazimika, aliongea siku anateua.

Unajua bhana! Uhusiano wa mteuaji na mteuliwa au mtenguliwa umejengwa katika usiri mkubwa sawa na ule wa wana ndoa. Mkiachana huwezi kusema alikuwa ananuka kikwapa. Akijibu?! Kujibu kushindwe na kulegea.

Kazi ya serikali siyo ya mtu mmoja. Kwa hiyo kutueleza kazi ya mmoja hakutupatii picha ya kutosha. Wapo wanaokwamishwa na wasiowajua. Ziko wizara zinaingiliana. Watoto wa shule (Elimu) wakicheza mpira (Michezo). Wasipocheza vizuri atumbuliwe nani?

Hili ni gumu. Wazembe na wasiotosha, wabadilishwe tu, lakini tujue, mabadiliko yakiwa mengi na ya mara kwa mara, wazushi watasema tatizo ni la mteuaji. Watabwata, "Hakuna", "hatoshi", "ashindwe" nk. Hakuna chuo cha uwaziri. Semina elekezi moja haitoshi. Mkataba wetu ni mbovu. Eti sharti awe mbunge! Kweli? Mnaochelewesha mkataba mpya mnasababisha boss ajiadhibu.

Niliota siku moja naenda kutekeleza ahadi niliyompa mke wa waziri yule Mjaluo. Nikaota nikjibiwa na boss kubwa, "Nenda kawaambie, sihitaji kura zao ili niwe boss wao!"

Sikumuita mke wa Mjaluo kumpa jibu baada ya kukumbuka kuwa ni ndoto tu. Nilisahau hata mlango ulioniingiza ofisi ya boss, nikaingia washroom. Akabaki ananicheka. Nami nikajifanya nilikuwa na haja wakati nimekosea njia.

Nina mpango wa kustaafu kuwatania Wajaluo. Kuna mtu mzito amenionya nikaonyeka. Nahitaji maoni yao inbox ili nifanye uamuzi.

Narudia tena; ikibaki ni siri tutanufaika wote.

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***



Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA

Kona ya Dkt. Bisimba

# Tanzania na uhalisia wa kinara wa uchumi EAC

WIKI iliyopita zilitimia siku 100 tangu ngwe ya pili ya serikali ya awamu ya sita kuingia madarakani ikiwa imegubikwa na kadhia kubwa.

Serikali imejinasibu kuwa katika siku hizo 100 mambo mengi yameshafanyika ili kutekeleza ahadi zilizotolewa awali.

Wakati hayo yakiendelea, tumepata taarifa kuwa Tanzania inaelekea kuwa kinara wa uchumi Afrika Mashariki, ikiipiku Kenya.

Inaelezwa kuwa Tanzania inafikia hatua hiyo kutokana na ongezeko la uzalishaji wa dhahabu, ikishika nafasi ya nne Afrika, ubora wa miundombinu hasa ya usafirishaji kama vile reli ya kisasa (SGR) na barabara bora pamoja na huduma za kisasa za fedha.

Kwenye utalii ndiyo usiseme, yapo maeneo mengi ya kuvutia watalii; Serengeti, Zanzibar na hata Kilimanjaro, Bandari ya Dar es Salaam kwa biashara ni nambari moja.

Ukiyasoma haya yanafurahisha kabla hujawasikiliza Watanzania wenyewe wanaouishi huo ukweli wa kiuchumi.

Maana ya uchumi wa nchi au hata wa mtu binafsi, ni kiasi unachoweza kumletea manufaa na maendeleo katika mabadiliko ya maisha.

Je, inatosha kujigamba kuwa tuko vinara wa kiuchumi wakati maisha ya watu wengi hayaakisi hali halisi?

Kwanza tuitazame bajeti ya nchi ambayo kwa sehemu kubwa inaonekana kuelekezwa kwenye kulipa deni la taifa na kwenye miradi mikubwa.

Labda siyo vibaya kulipa madeni, lakini haya madeni na hii miundombinu inayoendelezwa tunaitafsiri vipi katika eneo la kuboresha kipato cha mwananchi ambacho ni cha chini sana?

Kila uchao tunasikia malalamiko ya ukosefu wa ajira, nafuu ya maisha haionekani kwani watu wengi wanaonyesha wanavyopata dhiki hata kujikimu kwa mlo mmoja kwa siku.

Ukiangalia bajeti haina ulinganifu katika sekta ambazo hasa zinagusa maisha ya watu, sekta ya afya na elimu ambazo ni nguzo ya ustawi wa jamii.

Pamoja na ukinara wa uchumi unaoelezwa, bado nchi inakabiliwa na upungufu mkubwa wa huduma muhimu kama dawa hospitalini.

Zipo shule nyingi zisizo na walimu wa kutosha huku walimu wahitimu ualimu wakizurura bila ajira.

Ukizungumza na waajiri nao wana kilio chao kuwa wapo vijana wengi wahitimu, lakini changamoto ni ujuzi walionao usioendana na mahitaji ya soko.

Siyo ajabu kuwaona wahitimu wa vyuo vikuu wakiendesha bodaboda au magari madogo ya abiria.

Kama ni kweli tunakua kiuchumi kama inavyoelezwa, hizi changamoto nazo zionekane kupatiwa ufumbuzi wa muda mrefu.

Katika suala hili la kiuchumi pia kuna kujiuliza hali ya mfumo wa kodi. Mzigo wa kodi umeegemea wapi? Kwa walaji na wafanyabiashara wadogo kwa njia za kodi zisizo za moja kwa moja au vipi?

Ninavyosikiliza sauti hii ya kukua kiuchumi, sioni mkakati wa wazi na ulio imara kukuza uwanda wa walipa kodi bila kudidimiza shughuli ndogondogo za kiuchumi kama mama lishe, machinga n.k.

Haya yangeonekana kwenye bajeti ambayo ni nyenzo ya jamii na kulenga kudhibiti gharama za maisha kupanda.

Ukinara wa uchumi kipimo chake kinapaswa kuwa unafuu wa maisha kwa wananchi. Vigezo visiwe miundombinu tu, bali sura ya wananchi ndiyo izungumze na huo ndiyo uwe ujasiri wetu katika kujiinua kama vinara wa uchumi Afrika Mashariki.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

Habari

# Lissu ashangaza



*Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu, akifurahia jambo akiwa katika kizimba cha Mahakama Kuu kwa ajili ya kusikiliza kesi yake ya uhaini katika mahakama hiyo, Dar es Salaam juzi. (Na Mpigapicha Wetu).*

Na Mwandishi WETU

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Antipas Lissu, ameendelea kuwa korokoroni kwa zaidi ya miezi 10, lakini bado "ni yuleyule."

Licha ya kuwa mpweke ndani ya Gereza la Ukonga, Dar es Salaam, Lissu bado anapenda kutabasamu. Sura yake imejaa bashasha na kunawiri. Haonekani kuchoka wala kujaa hasira zinazoonekana waziwazi.

Tangu alipokamatwa Aprili 9,2025, wilayani Mbinga, Mbeya na kufunguliwa kesi ya uhaini jijini Dar es Salaam, Lissu, sasa ametimiza zaidi ya miezi kumi akiwa korokoroni.

Endapo Lissu atapatikana na hatia, atakabiliwa na adhabu ya kunyongwa hadi kufa.

Pamoja na tishio la adhabu hiyo, Lissu amekuwa tofauti mno na washitakiwa wengine wanaofikishwa mahakamani wakikabiliwa na shitaka hilo, Lissu anaonekana kuishinda hofu na sura yake haionekani kuwa na dalili za kukata tamaa.

Washtakiwa wengi ambao hukabiliwa na mashitaka makubwa – ikiwamo ya kuua, ambayo yanabeba adhabu ya kifo, huangua vilio mahakamani kama njia ya kutaka huruma kwa majaji wanaosikiliza kesi zao.

Wengine hupoteza nuru usoni kila wanapokumbuka mwelekeo wa kesi zao, wengine hugoma kula na kunywa mara kwa mara na wengine hupoteza uzito na afya zao kuteteleka kwa sababu tu pindi watakapopatikana na hatia, watahukumiwa kunyongwa hadi kufa.

Kutokana na hali hiyo, mwanasiasa huyo – Lissu, anaendelea kushangaza watu kutokana na jinsi anavyoonekana mahakamani kila shauri lake linapotajwa.

Mara zote Lissu amekuwa ni mtuhumiwa wa kipekee kwani anaonekana mwenye furaha tofauti na washtakiwa wengine wengi.

Tangu shauri hilo lilipokuwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kwa hatua za awali za usikilizwaji, Lissu hakuwahi kunyong'onyea, hakuwahi kuonyesha kusikitishwa na kesi hiyo, wala hajawahi kuonyesha hofu dhidi ya shtaka hilo.

Hali hiyo imekuwa ikizua maswali na mijadala mingi katika mitandao ya kijamii ambapo sehemu ya wachangiaji hushangazwa na ujasiri wa mwanasiasa huyo ambaye anaishi na risasi mwilini baada ya kunusurika katika jaribio la kushambuliwa na risasi miaka tisa iliyopita.

**Anavyosalimia wafuasi**

Katika Mahakama Kuu ambako shtaka lake linasikilizwa, Lissu amekuwa akiingia mahakamani akiwa na "furaha iliyopitiliza" utadhani haishi mahabusu.

Pamoja na kutabasamu na kucheka mara kwa mara afikapo mahakamani, amekuwa akiwapungia mikono wafuasi wake na wakati mwingine 'kuwabusu hewani' kwa furaha.

Pia, huonyesha alama ya mshikamano kwa kukunja ngumi ya mkono wa kulia uliofungwa Rozali na kuzungusha mkono mara kadhaa hewani huku wasikilizaji na wafuasi wake wakiitikia kwa kukunja ngumi na kuzungusha mikono hewani.

**Afya yake ilivyo**

Wakati anakamatwa miezi kumi iliyopita, Lissu alikuwa amenawiri, lakini hadi sasa afya yake haionekani kudorora licha ya kuishi mahabausu kwa kipindi chote hicho.

Inaendelea Uk. 13

# Lissu ashangaza

Inaendelea Uk. 12

Mwanasiasa huyo bado ni yuleyule, sura yake inang'aa na anaonekana mwenye afya njema, jambo ambalo ni mara chache kuliona kwa washtakiwa wa kesi nzito zinazoweza kugharimu maisha ya mtuhumiwa pindi atakapopatikana na hatia.

### Anavyobeba vitabu

Kitaaluma, Lissu ni mwanasheria na katika shtaka lake hilo, anajitetea mwenyewe ambapo anakabiliana vilivyo na mawakili saba wa upande wa Jamhuri wakiongozwa na mawakili wakuu wa serikali.

Jambo linalowashangaza wengi na ambalo ni mjadala mkubwa katika mitandao ya kijamii ni jinsi anavyoingia mahakamani akiwa amebeba mifuko mitatu ya vitabu sambamba na nyaraka zingine za kisheria ambazo amekuwa akizitumia katika kesi hiyo.

Kila anapofika kizimbani, hutoa vitabu na nyaraka hizo na kuzitandaza katika meza ya kizimba ambapo hutumia kitabu au nyaraka moja moja kila anapokuwa akihitaji kuzitumia wakati wa kujitetea.

Kila anapoingia mahakamani, huonekana akiwa amebeba mfuko mmoja katika bega la mkono wa kushoto na mfuko mmoja huwa ameushikilia kwa mkono wa kushoto na mfuko mwingine huwa mkono wa kulia.

Hata hivyo, mara kadhaa mshtakiwa huyo huonekana akilemewa na mizigo hiyo hasa anapokuwa akipanda na kushuka kwenye ngazi za jengo la ghorofa la mahakama hiyo.

### Alalamikia kunyimwa chakula

Februari 12, 2026, majira ya mchana ni siku nyingine ambayo itaingia katika kumbukumbu za mahakama kuu hiyo baada ya Lissu kuwaambia wafuasi wake, kwamba alinyimwa chakula cha mchana.

Tukio hilo ambalo wasikilizaji, maofisa wa mahakama, mawakili na majaji hawakulitarajia, lilisababisha baadhi ya wanawake kulia na wengine walizimia wakionyesha kuumizwa na jambo hilo.

Wakati Lissu anaanza kuzungumzia chakula, awali suala hilo lilionekana kama mzaha kwani alipowauliza wasikilizaji kama wameshakula, wao walimjibu kwa furaha, kwamba washakula na wameshiba.

Walipomjibu hivyo, yeye aliwaambia huku akitabasamu, "mimi mwenyekiti wenu sijala." Kauli hiyo ilibadilisha upepo ghafla mahakamani hapo kwani wanawake waliangua vilio na wengine walizimia.

Watu wengine ambao wengi wao ni wafuasi wa Chadema, waliwashutumu askari Magereza na kuwanyooshea vidole kwa kutompa chakula mshtakiwa ingawa ni haki yake.

Suala hilo lilihitimishwa na mmoja wa majaji watatu wanaosikiliza kesi hiyo, Jaji Danstan Ndungulu ambaye aliamua kuahirisha kesi hiyo.

Pia, Jaji Ndungulu aliwaagiza askari hao kuhakikisha kuwa Lissu hakosi huduma ya chakula. Alisema; "kumnyima chakula mshtakiwa ni kukiuka haki za binadamu."

### Nje ya mahakama

Maisha ya kisiasa ya Tundu Lissu, yamejaa misukosuko na vitisho vya kukatisha tamaa.

Hiyo inatokana na madhila ambayo amekuwa akipitia kabla na wakati alipokuwa Mbunge wa Singida Mashariki kupitia Chadema hadi wakati huu ambapo anakabiliwa na kesi ya uhaini.

Pamoja na madhila, misukosuko na mambo kadhaa yanayotishia uhai wake, Lissu hajawahi kuonyesha kurudi nyuma, hajawahi kuonyesha uoga wala kusalimu amri, badala yake ameendelea kuwa sehemu ya wakosoaji wakuu wa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Amekamatwa mara kadhaa na kufunguliwa kesi enzi za uongozi wa Rais Jakaya Kikwete na hali ikawa mbaya zaidi kwake baada ya Rais John Magufuli kuingia madarakani mwaka 2015.

Wakati maisha yake yakiendelea kutikiswa, Lissu ni miongoni mwa wanasiasa maarufu na wenye ushawishi katika jamii huenda kutokana na jinsi anavyojiamini.

Inaendelea Uk. 14

## Habari

# Lissu ashangaza

Inatoka Uk. 12

Septemba mwaka 2017, alipokuwa akihudhuria vikao vya Bunge jijini Dodoma. Risasi 16 ziliingia mwilini mwake na kuuchanachana, kisha alifanyiwa upasuaji mkubwa Nairobi, Kenya na Ubelgiji. Dakika chache baada ya kupigwa risasi, alitibiwa katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, baadaye alihamishiwa katika hospitali moja jijini Nairobi, Kenya ambako alilazwa kwa miezi minne kabla hajahamishiwa nchini Ubelgiji kwa matibabu zaidi.

Wakati akiendelea na matibabu, alizidi kutikiswa zaidi kwani serikali iligoma kugharamia matibabu yake ingawa alikuwa na haki hiyo kisheria.

Akiwa katikati ya matibabu huku akipigania uhai wake, iliyokuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ilimfuta ubunge na kutangaza Jimbo la Singida Mashariki alilokuwa akiliongoza, kuwa liko huru na uchaguzi mdogo ulifanyika.

Shambulizi la risasi dhidi yake liliitikisa nchi, wapo watu waliomlilia, wengine walimuombea makanisani na misikitini, lakini Serikali ya Rais Magufuli, ilipiga marufuku maombi ya pamoja ya kumuombea kwa Mwenyezi Mungu ili apone haraka.



*Wafuasi wa Chadema wakiangua vilio baada ya mwenyekiti wao, Tundu Lissu, kudai hajapewa chakula wakati wa kusikiliza kesi ya uhani katika Mahakama Kuu, Dar es Salaam juzi. (Na Mpigapicha Wetu).*

### Kesi ilipokuwa Kisutu

Wakati kesi yake ya uhaini ikiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi, Kisutu, wananchi wakiwamo wafuasi wa Chadema, walikuwa wakifurika katika mahakama hiyo.

Askari Polisi walikuwa wakiwapiga na kujeruhi baadhi ya wananchi waliokuwa wakifika mahakamani hapo, ambapo baadhi yao walivunjwa miguu, mikono, mbavu na wengine waliumizwa.

Awali, Lissu alikuwa akitetewa na mawakili 32 maarufu nchini waliokuwa wakiongozwa na Mwanasheria Mkuu wa Chadema, Dkt. Rugemeleza Nshala wakati Jamhuri ilikuwa ikiwakilishwa na mawakili saba.

Hata hivyo, katika hali ambayo wengi hawakuitarajia, Juni 16, 2025, Lissu aliwaweka pembeni mawakili wake wote kutokana na sababu alizosema kuwa ni mawakili wake kutopewa uhuru wa kumtetea na kumtembelea anapokuwa mahabusu anakoshikiliwa.

Kuanzia siku hiyo, alianza kujitetea mwenyewe na hapo ndipo alipoanza kuonyesha uwezo wake kisheria.

### Kesi yake inavyofuatiliwa

Wakati shauri hilo likiunguruma katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, awali lilikuwa likionyeshwa mubashara na vyombo vya habari ambapo wananchi walikuwa wakijaa katika vibanda vya kuonyesha mpira (maarufu kama vibandaumiza), ili kushuhudia mwenendo wa kesi hiyo. Kama ambavyo mashabiki wa soka hulipa viingilio kushuhudia soka katika vibandaumiza hivyo, wananchi hao pia walikuwa wakilipa viingilio ili kushuhudia mnyukano wa kisheria kati ya wanasheria wa Lissu dhidi ya mawakili wa Serikali, mnyukano kati ya Lissu na mawakili wa Serikali na mnyukano kati ya Lissu na mashahidi wa Jamhuri.

Katika vijiwe vya kawaida mitaani, katika vyombo vya habari ikiwamo mitandao ya kijamii na kwenye vyombo vya usafiri, habari kuu imekuwa ni kesi ya uhaini inayomkabili Lissu.

Wananchi wanaichambua vilivyo kesi hiyo, wanamchambua Lissu kama mshtakiwa na wengine wanaichambua Serikali huku wakitoa mapendekezo kadhaa.

# Wizi washamiri hospitalini

**Na Mwandishi WETU**

MATUKIO ya wizi katika baadhi ya hospitali nchini yakihusisha vyumba vya kuhifadhia maiti na maeneo ya kupumzikia, yamekithiri, Pambazuko linaripoti.

Baadhi ya watu waliokumbwa na kadhia hiyo wamelieleza Pambazuko jinsi wizi huo unavyofanyika na kusema hali hiyo imeibua taharuki kwa watu wanaouguza wagonjwa na wafiwa wanaofika hospitalini.

Pambazuko limezungumza na Pulkeria Mtui, mmoja wa watu waliokumbwa na kadhia ya kuibiwa katika eneo la mochwari ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam wakati wa kuchukua mwili wa kijana wake.

Pulkeria amesema; "Nikiwa katika majonzi makubwa alikuja mwanamke mmoja akiwa amevaa gauni jeupe kama nililokuwa nimevaa mimi. Nilivyomuona nikaamini ni mmoja wa waombolezaji. Alinishika mkono kisha akanipangusa machozi…"

"Baada ya muda akanipokea pochi, sikuwa na hofu kwa sababu kwanza alikaa na mimi kwa muda mrefu. Wakati mwili wa kijana wangu unatolewa mochwari yule mama aliinuka na kunirudishia pochi na kuondoka."

Pulkeria anasimulia kuwa akiwa njiani kuelekea nyumbani kwao maeneo ya Madale Nguzo, jijini Dar es Salaam, alifungua pochi yake na kubaini kuwa simu na kipochi kidogo kilichokuwa na fedha havimo.

Anasema aliwauliza ndugu zake wa karibu kuhusu mwanamama yule nao walisema hawamjui na walidhani ni rafiki yake wa karibu.

Mwanakheri Jumaa naye ni miongoni mwa waliokumbwa na masahibu hayo katika hospitali hiyo, ambaye anakwenda hapo mara kwa mara akimuuguza ndugu yake.

"Kuna siku nilikuwa nimepitiwa na usingizi nikiwa kwenye eneo la mapumziko. Mwanamke mmoja alikuja kulala jirani yangu, pembeni yangu niliweka kibegi kikiwa na nguo za mgonjwa na zangu…"

"Ilipofika saa tisa usiku nilishtuka sikumuona yule mwanamke na begi pia halikuwepo!" anasimulia na kuongeza: "Niliwashtua wenzangu kuwa nimeibiwa na mmoja akasema naye kaibiwa mfuko wenye nguo na simu. Kwa kifupi sisi wauguzaji hasa tunaotoka mikoani tunashida sana."

Naye Jackyline Peter, aliyekuwa anamuuguza mama yake katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, amedai kuwa aliibiwa nguo za mgonjwa usiku akiwa amelala.

Mmoja wa washirika wa Kanisa la Inuka na Uangaze, aitwaye Regina Lawrence, amesema waumini wa kanisa hilo wanalazimika kupeleka misaada hususani nguo ili kuwasitiri wagonjwa na wauguzaji hospitalini.

"Tumepita baadhi ya hospitali hapa Dar es Salaam kutoa misaada. Tunapokwenda tunakutana na visa vya watu wengi kuibiwa vitu vyao. Jamani wenzetu wanaouguza wanateseka, kuna watu wanaibiwa nguo na viatu, kama una chochote tuwasaidie," amesema Regina.

Ofisa Habari wa Hospitali ya Mloganzila, Neema Mwangomo, amesema hospitali hiyo haina taarifa hizo za wagonjwa na wauguzi kuibiwa.

"Hizi taarifa nazisikia kutoka kwenye gazeti lenu. Lakini tumezipokea na tutazifanyia kazi," alisema.

Mmoja kati ya viongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Amana, ambaye hakutaka jina litajwe amedai kuwa matukio ya wizi yalikuwapo kipindi cha nyuma ila kwa sasa yamedhibitiwa.




***Mkurugenzi Mtendaji wa Equity For Tanzania Limited (EFTA), Nicomed Bohay (kushoto), akiongoza mazungumzo kwa wageni waalikwa wakati wa uzindunzi wa Hati Fungani za EFTA zenye thamani ya shilingi bilioni 50 kwa ajili ya masoko ya mitaji na sekta halisi za uzalishaji kilimo, usafirishaji na viwanda, halfa hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.(Na Mpigapicha Wetu)***

■ Habari

# Mwafaka SUK Zanzibar wanukia



*Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo, Othman Masoud Othuman, akisalimia viongozi na wanachama wa chama hicho kutoka Micheweni na Wete, Pemba wakati wa ziara ya kueleza mwelekeo wa mazungumzo ya kutafuta muafaka wa kudumu, hivi karibuni. (Picha na ACT)*

**Na Mwandishi WETU, Unguja**

BAADA ya juhudi zilizowahusisha vigogo kadhaa, wakiongozwa na marais wastaafu, sasa mahasimu wa kisiasa Zanzibar, wanaelekea kukubaliana kufanya kazi pamoja.

Mwafaka kati ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ACT Wazalendo Zanzibar unatarajiwa kufikiwa hivi karibuni na kukiwezesha chama hicho cha upinzani kujiunga kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Sasa ni rasmi kwamba chama cha upinzani cha ACT Wazalendo kinatarajia kuingia na kushiriki kwenye SUK, baada ya kazi kubwa ya upatanishi iliyokuwa ikifanyika chini chini tangu Novemba mwaka jana, Pambazuko linaweza kueleza kwa kina.

Baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka jana 2025, ACT Wazalendo kilikataa kuyakubali matokeo ya uchaguzi huo visiwani Zanzibar na kukacha kujiunga kwenye SUK na kuzifanya nafasi za uwaziri zilizotengwa kwa ajili ya chama hicho ndani ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kubaki wazi hadi leo.

Hali hiyo ilizusha sintofahamu na kutishia kusambaratisha SUK, hasa pale ACT kiliposisitiza kuwa hakitaingia kwenye serikali hiyo mpaka matakwa yake kuhusiana na masuala mbalimbali yasikilizwe na kukubaliwa.

Mwenyekiti wa chama hicho cha upinzani, ambaye pia alikuwa mgombea urais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, almaarufu OMO, alitangaza kutoyatambua matokeo hayo ya uchaguzi na kueleza msimamo wa chama hicho kutojiunga na SUK kutokana na kile alichoeleza kuwa udanganyifu mkubwa katika uchaguzi huo.

Hata hivyo, taarifa ambazo Pambazuko linazo zinasema siku yoyote kuanzia sasa vingozi wa CCM na ACT Wazalendo watakuja hadharani kutangaza makubaliano yaliyofikiwa kati yao ili kuinusuru SUK isisambaratike.

Hatua hiyo imetokana na kuwapo mazungumzo ya kina yaliyoshirikisha vyama hiyo vya siasa upande wa Zanzibar kwa lengo la kutafuta muafaka wa msigano wa kisiasa uliotokea baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 na 29, 2025.

Tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu huo kulikuwepo na sintofahamu juu ya hatma ya SUK, ambapo tangu wakati huo hadi sasa ACT Wazalendo kiligoma kuwasilisha majina manne kwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi ili aweze kuwateua kushika nafasi za uwaziri kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar.

Aidha, chama hicho hakijawasilisha jina la mtu ambaye atashika nafasi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kama inavyoeleza Katiba ya Zanzibar.

Chanzo cha uhakika kutoka Zanzibar, kimeliambia Pambazuko kuwa mazungumzo kati ya vyama hivyo viwili yalianza tangu Novemba 5 mwaka jana 2025 kwa kuwashirikisha marais wastaafu; Amani Abeid Karume na Dkt. Mohammed Shein kwa upande wa CCM, huku ujumbe wa ACT ukiongozwa na Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Othman Masoud Othman pamoja na Mwenyekiti mstaafu wa chama hicho, Juma Duni Haji.

Inaendelea Uk. 17

# Mwafaka SUK...

Inaendelea Uk. 16

Mbali na viongozi hao wa kisiasa, pia walikuwepo wataalamu wa sheria na Katiba kwa ajili ya kuweka sawa kile kitakachohitaji ufafanuzi kwenye maeneo hayo.

"Mojawapo ya agenda za vikao hivyo vya muafaka ni majukumu rasmi ya nafasi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, ambayo kwa sasa ni kupambana na dawa za kulevya, pamoja masuala ya mazingira.

"Lakini pia mazungumzo yalihusisha mifumo ya uchaguzi ambapo Othman alieleza bayana kwamba muafaka huo ulenge kuondoa hofu ambayo inawakumba wananchi kila uchaguzi wa Zanziabar unapofika..."

"ACT imetaka kushughulikiwa na kuondolewa kwa mazingira yote yanayoashiria wizi wa kura ikiwemo suala la kura ya mapema pamoja na umuhimu wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kushirikisha wadau wengine ili kujenga uaminifu kwayo," alisema mtoa habari wetu.

### CCM yakubali

CCM kwa upande wake kimesema mazungumzo yake na ACT Wazalendo yanaendelea, na yakikamilika yatawekwa hadharani kwa wananchi.

Katibu wa Idara ya Itikadi Uenezi na Mafunzo CCM Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis, amesema mazungumzo hayo yanaelekea kuzuri na wakati wowote kuanzia sasa wananchi watajulishwa kinachoendelea.

"Mazungumzo yanaendelea vizuri. Wenzetu walilalamika na sisi CCM ni kawaida yetu kusikiliza, na hili hatujaanza leo, na waanzilishi wa haya mnamjua Amani Abeid Karume alipokutana na Maalim Seif wakati huo, baadaye vikao vya CCM vikapitisha, hili si jambo geni kukaa na kuzungumza," alisema Mbeto alipozungumza na Pambazuko.

### Wanachama ACT Wazalendo

Wakizungumza katika mkutano uliohutubiwa na OMO Januari 11, 2026, wanachama wa ACT Wazalendo wamesema wako tayari kupokea uamuzi wowote utakaofikiwa na viongozi wao katika juhudi za kutafuta muafaka wa kudumu wa kisiasa Zanzibar.

Akizungumza kwa niaba ya wanachama huko Wete Pemba, Mratibu Rashid Ali Abdallah alimhakikishia Othman kuwa wanachama wana imani kamili na uongozi wake.

"Ndugu Mwenyekiti, sisi wanachama wako hatuna shaka na wewe pamoja na viongozi wenzako. Tuko tayari kupokea maamuzi yoyote mtakayotuletea," alisema Rashid.

Mwenyekiti wa ACT Mkoa wa Wete, Juma Khamis Ali maarufu Kabakaba, alisema yeye pamoja na wanachama wa mkoa huo hawana shaka na uamuzi utakaofanywa na viongozi wa kitaifa.

### Jussa anena

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Zanzibar, Ismail Jussa Ladhu, amesema imani wanayoionyesha wafuasi wa chama hicho kwa viongozi ndio inayosababisha chama hicho kunawiri kila uchao.

Aidha, kwa upande wake, Othman alisisitiza umuhimu wa Wazanzibar kuwa kitu kimoja bila kujali tofauti za vyama vya siasa.

Alisema migogoro ya kisiasa huwapa nafasi maadui kuingiza maslahi yao na kusisitiza kuwa umoja ni muhimu kwa ustawi wa taifa.

"Lazima Wazanzibari tuwe kitu kimoja na tulinde nchi yetu ili adui asipate nafasi. Lengo la mazungumzo hayo ni kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) itakayojenga mshikamano na kupigania maslahi ya wananchi," alisema.

Othman pia aliishukuru timu ya mazungumzo ya chama hicho iliyoongozwa na Mwenyekiti mstaafu, Juma Duni Haji,

Alisema katika mazungumzo hayo pande zote zimekubaliana kurejea katika vyama vyao kukamilisha taratibu za ndani kabla ya kutoa taarifa ya pamoja, huku wakiahidi kurejesha imani ya wananchi kwa vitendo kupitia utekelezaji wa makubaliano yatakayofikiwa.

Miongoni mwa mambo yaliyokubaliwa ni pamoja na kutungwa kwa Katiba mpya, kuhakikisha utawala wa sheria unazingatiwa.

Mengine ni mamlaka kubaki mikononi mwa wananchi, kuimarisha mfumo wa uwajibikaji kwa viongozi na kufanyia mapitio mfumo wa uchaguzi ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima.

Mbali na hayo, kutakuwa na utaratibu maalumu wa utekelezaji wa makubaliano hayo mara baada ya taratibu za ndani za pande zote kukamilika.

Habari

# Rais Samia aliahidi, amefanikisha




*Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia Kikao cha Umoja wa Afrika katika mkutano wa 39 wa wakuu wa nchi na serikali wa Umoja wa Afrika (AU), uliofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia, juzi. (Picha na Ikulu).*

Na Mwandishi WETU

WIKI iliyopita Rais Samia Suluhu Hassan alitimiza siku 100 za utawala wake huku akifanikisha ahadi kadhaa alizoeleza kuzitekeleza ndani ya kipindi hicho baada ya kuapishwa.

Yapo mambo ambayo Rais Samia aliahidi kupitia ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na mengine kuwamo kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa'

Miongoni mwa ahadi zilizotekelezwa ni pamoja na kutoa ahueni kwa wananchi wenye kipato cha chini kuruhusiwa kuchukua miili ya watu waliofariki dunia wanaodaiwa ankara za matibabu hospitali.

Akizungumza na gazeti hili, Abdalla Hamisi, ambaye amefiwa na mama yake mzazi aliyekuwa akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala, Dar es Salaam, amesema wamenufaika na agizo la Rais Samia la kutozuia miili kutokana na madeni ya matibabu.

"Kwa muda mrefu mama yangu alikuwa anaumwa alilazwa hapa Mwananyamala. Tumetumia fedha nyingi kumtibu, mwishoni tulilemewa tulishindwa kumudu gharama, mama yetu amefariki…"

"Tunamshukuru sana Rais Samia licha ya kuwa tunadaiwa hapa hospitali, lakini tumechukua mwili wa mama yetu tunajiandaa kwenda kumuhifadhi," anasema Hamisi ambaye hakutaka kutaja kiwango cha fedha wanachodaiwa.

Mmoja kati ya madaktari wa hospitali hiyo ambaye hakuwa tayari kutaja jina kwa madai kuwa "siyo msemaji wa sekta ya afya" amesema ahadi ya Rais Samia inatekelezwa kama ilivyoelekezwa.

"Kwa kuwa serikali imewajali wananchi nashauri familia ambazo zinatakiwa kulipia gharama za matibabu za ndugu zao waliofariki, basi nao watimize wajibu wa kulipa madeni hayo kwa wakati ili huduma za afya ziendelee kutolewa kwa ufanisi zaidi," anasema Daktari huyo.

### Bima ya afya kwa wote

Ahadi nyingine ambayo utekelezaji wake umeanza kuonekana ni Bima ya Afya kwa Wote.

Katika kipindi cha siku hizo 100 serikali imeanza utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Utekelezaji wa mpango huo umeanza kwa kusajili wananchi, hasa makundi maalum katika awamu ya majaribio.

Wanaolengwa katika uandikishaji huu wa awamu ya kwanza ni makundi ya wazee, watoto, wajawazito na watu wenye ulemavu.

Majaribio hayo yamelenga kutathmini utekelezaji wa mpango huo ili kubaini changamoto zinazoweza kujitokeza na kuzitafutia ufumbuzi.

### Ajira zamwagwa

Aidha, serikali imetimiza ahadi ya kuwaajiri watumishi 5,000 na kuwapangia vituo vya kazi katika maeneo mbalimbali nchini.

Wengi wa waajiriwa wapya ni katika sekta za afya na elimu.

Kwa upande wa elimu hadi sasa walimu 7,000 wameshaajiriwa, huku mpango mkakati wa kisayansi wa kujenga umahiri wa kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK), kwa watoto wa elimu ya awali na darasa la kwanza hadi la pili ukiwa umezinduliwa rasmi na Rais Samia.

Akizundua mpango huo Rais Samia ameziagiza mamlaka husika kuhakikisha mpango huo unatekelezwa kwa vitendo ili uwe na tija kwa taifa.

Inaendelea Uk. 19

# Rais Samia aliahidi...

Inaendelea Uk. 18

**Magonjwa sugu bado**

Hata hivyo, hadi sasa Wizara ya Afya bado haijaeleza bayana hatua ya utekelezaji wa ahadi ya kugharamia kwa asilimia 100 wagonjwa wenye magonjwa yasiyoambukizwa yakiwamo saratani, kisukari, figo, moyo na mishipa ya fahamu.

Pambazuko lilipomtafuta Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Wizara ya Afya, John Mapepele, ili kueleze utekelezaji wa ahadi hiyo, alimtaka mwandishi kuwasiliana na Mganga Mkuu wa Serikali, Dkt. Grace Maghembe ambaye jitihada za kumpata zinaendelea kwa kuwa wiki iliyopita hakupatikana kwa namba yake ya simu na ofisini hakuwepo kwa maelezo kwamba ana “majukumu nje ya eneo lake la kazi.”

**Wajasiriamali**

Serikali pia imetimiza ahadi kwa kutoa shilingi bilion 200 kwa ajili ya mitaji ili kuwawezesha kiuchumi wafanyabiashara wadogo na wa kati na kampuni changa.

Hata hivyo, baadhi ya madereva wa bodaboda na bajaji wamedai kuwa hadi sasa maelekezo ya Rais Samia ya kurasimisha sekta zisizo rasmi ili ziingizwe kwenye mfumo rasmi wa serikali haujawafikia.

“Tulisikia kuwa ndani ya siku 100 tutaingizwa kwenye mfumo rasmi ili na sisi tunufaike na fursa zinazotolewa na serikali za kupata mikopo, lakini hadi sasa hatujaingizwa licha ya kituo chetu kusajiliwa,” amesema Kiongozi wa Madereva wa Bodaboda Tegeta Kibaoni, Faustine Basso.

Naye Godfrey Magoire, dereva wa bajaji kituo cha Msigani, Kata ya Wazo Hill, anasema licha ya kituo chao kusajiliwa hata hivyo fursa ya kupata mikopo inayotolewa na serikali haijawafikia.

Ameiomba serikali kuona namna bora ya kuvifikia vituo vyote ili fursa hiyo itolewe bila upendeleo.

Kutokana na changamoto ya ukosefu wa maji nchini Rais Samia aliahidi kuanza kwa utekelezaji wa ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji ambayo vyanzo vyake vikuu vitatokana na Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

Waziri wa Maji Jumaa Aweso, ameeleza utekelezaji wa ahadi hiyo na kusema kuwa upembuzi yakinifu wa kuyatoa maji  Ziwa Victoria kuelekea jijini Dodoma tayari umeshakamilika.

Aidha, mchakato wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kuelekea mikoa ya Katavi - Rukwa hadi Kigoma umeshaanza ambapo mhandisi mshauri amekwishapatikana.

Kwa mujibu wa waziri huyo, mpango wa ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji umeanza kufanyiwa kazi kama ilivyoahidi Rais Samia.

**Mawaziri wajivuta?**

Pamoja na kutekelezwa kwa ahadi kadhaa, hata hivyo agizo la kuwataka mawaziri na wakuu wa mikoa kujibu maswali ya wananchi kwa njia ya kidigitali halijafanyiwa kazi.

Akizungumzia suala hilo, mkazi Dar es Salaam kutoka eneo la Sinza Kijiweni, Lulu Mwaitebela, anasema; “Bila shaka Rais Samia aliwataka mawaziri na wakuu wa mikoa kusikiliza kero zetu na kuzitatua…”

“Huu utaratibu ulikuwepo miaka iliyopita na kwa sababu viongozi hawa hawajatekeleza aliypoagiza basi Rais Samia awawajibishe.”

Aidha, Rais Samia aliahidi kushughulikia suala la maridhiano na kuanza kwa mchakato wa kuandikwa kwa Katiba mpya.

Katika hotuba yake ya mwaka mpya Rais Samia amesema serikali imejipanga kujenga umoja wa kitaifa, huku hatua za kuunda tume ya maridhiano zikianza kufanyiwa kazi.




iMbeJu
CRDB BANK foundation
Go Green na iMbeju Program
Call for Application
Window opened on
12th February 2026 to 11th March 2026
Scan to Register
For entrepereneurs to qualify:
Have a formal registered business or have a clear path to compliance
Have proven market traction
Generate consistent revenue or have a clear path to profitability
Have a scalable business model and a full-time committed team
Be ready to scale and attract investment
Businesses addressing climate, environment, and sustainability challenges
TACATDP
Food and Agriculture Organization of the United Nations
giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH
FursaHub

# Ithibati yaimarisha uaminifu sekta ya habari

**Na Mwandishi WETU**

BODI ya Ithibati ya Waandishi wa Habari (JAB) imesema utekelezaji wa mfumo wa ithibati kwa waandishi na watangazaji wa habari nchini ni hatua ya kimkakati ya kuimarisha uaminifu, weledi na ushindani.

Kwamba bodi hiyo imedhamiria kuhakikisha kuwa sekta ya habari inashiriki kikamilifu kwa kutoa mchango katika uchumi wa kisasa unaotegemea taarifa sahihi na zenye kuaminika.

Akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Vyombo vya Utangazaji (ABC) uliofanyika Februari 13, 2026 jijini Dodoma, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa JAB, Wakili Patrick Kipangula, amesema ithibati inalenga kujenga taaluma yenye misingi imara ya kitaaluma, maadili na uwajibikaji kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229.

Wakili Kipangula, alisema ithibati siyo chombo cha kudhibiti maudhui, bali ni utaratibu wa kuweka viwango vinavyolinda hadhi ya taaluma na kuimarisha imani ya umma kwa vyombo vya Habari.

Amesema kwamba katika mazingira ya sasa ya ushindani wa kidijitali, uaminifu wa chanzo cha habari ndiyo mtaji mkubwa wa chombo husika.

Kipangula ameongeza kuwa vyombo vya utangazaji vinavyowekeza katika weledi wa rasilimali watu wake, vinajiweka katika nafasi bora ya kuvutia wawekezaji, matangazo na ushirikiano wa kimataifa, kwa kuwa soko la habari linazidi kuthamini ubora na uwajibikaji.

Kwa upande wa wadau wa mkutano huo ulioandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imeelezwa kuwa ushirikiano kati ya msimamizi wa maudhui na wadau wa tasnia ni nguzo muhimu katika kujenga sekta imara, inayochochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.



*Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa JAB, Wakili Patrick Kipangula akizungumza na waandishi wa Habari mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. (Picha na Mpigapicha Wetu).*

Hatua ya kuimarisha ithibati inaonekana kuwa sehemu ya mkakati mpana wa Serikali wa kukuza taaluma za ubunifu na mawasiliano kwa viwango vinavyokidhi mahitaji ya kitaifa na kimataifa, huku ikihakikisha kuwa sekta ya habari inabaki kuwa mhimili wa uwazi, uwajibikaji na maendeleo endelevu.

Waandishi zaidi ya 3,200 kati ya 3,900 walioomba vitambulisho vya uandishi wa habari (Press Card) wamethibitishwa baada ya kukidhi vigezo vya kisheria, hali inayoonesha mwitikio chanya wa wadau na utayari wa sekta kujiimarisha kitaaluma.

Barua Maalum

# Tunapinga Soko la Muleba kubadilishwa jina

**Mhariri,**

KWA heshima na taadhima, sisi wananchi – wengi wetu tukiwa wafanyabiashara wa Wilaya ya Muleba, Kagera, tunawasilisha rasmi maoni yetu kuhusu taarifa iliyosambazwa Februari 9, 2026 juu ya pendekezo la soko letu la Muleba kupewa jina la 'Magongo Complex.'

Jina hilo lilipendekezwa na Diwani wa Viti Maalum wa Kata ya Ijumbi, Tarafa ya Nshamba wilayani humu, Devotha Kemilembe Katabarwa.

Baada ya kufuatilia kwa kina tumebaini kuwa pendekezo hilo ni mbinu ya mhusika, Justus Magongo, kutaka jina lake litumike kwenye soko letu bila ridhaa ya wananchi.

Pendekezo hilo kwa ujumla halikuzingatia historia, utamaduni, wala matakwa ya wananchi wa Muleba, halikujali kwamba sisi wananchi ndiyo tumejenga soko hili kutokana na kodi zetu.

Anayependekeza na wale walioko nyuma yake hawajali kwamba tuliumia kwa muda mrefu bila kuwa na soko la kisasa linalobeba jina halisi linaloakisi eneo na mazingira yetu, yaani Soko Kuu la Muleba.

Sasa kwa niaba ya wananchi walio wengi tunatoa mapendekezo yafuatayo;

1. Soko letu liitwe rasmi Soko Kuu la Muleba, jina ambalo linaakisi utambulisho wa eneo letu na linaendana na utaratibu unaotumika katika maeneo mengi nchini.

2. Endapo kuna sababu maalum zinazofanya jina la 'Magongo' liwe na umuhimu kutumika katika miundombinu ya serikali, basi jambo hilo liangaliwe katika miradi mingine, kwa mfano moja ya wodi ya wagonjwa au chumba cha kingine chochote katika kituo cha afya kimojawapo wilayani Muleba.

Sisi wananchi wa Muleba, tunapenda kusisitiza kuwa, kwa kadri tulivyofuatilia, masoko mengi nchini yamepewa majina ya maeneo husika, siyo majina ya viongozi waliopo madarakani hasa wenyeviti wa halmashauri – kama ilivyo kwa Magongo.

Kwa msingi huo, tunaomba kwa heshima kubwa mamlaka husika ikiwemo Idara ya Mipango Miji, Mkurugenzi wa Halmashauri, Mkuu wa Wilaya ya Muleba na Mkuu wa Mkoa wa Kagera pamoja na wabunge, kulitupilia mbali wazo la kuliita soko letu "Magongo Complex" na badala yake kuthibitisha rasmi jina la Soko Kuu la Muleba.

Ni sisi wananchi kwa kushirikiana na wafanyabiashara,

**Wilaya ya Muleba,**
**Kagera.**



*Mafundi wa Dawasa Kinyerezi wakijaribu kuunganisha mabomba ya maji kwa ajili ya wakazi wa maeneo ya Mbezi, ambao wamekosa maji kwa zaidi ya miezi sita na kusababisha wananchi kutumia maji ya mabawa yasiyo salama kwa afya zao, Dar es Salaam hivi karibuni. (Na Mpigapicha Wetu)*



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

## Baadhi wahudumu SGR warekebishe kauli

**Mhariri,**
WIKI iliyopita nikiwa katika Stesheni ya Magufuli, Dar es Salaam nikisubiri usafiri wa treni ya kwenda Dodoma, nilishuhudia mhudumu wa SGR akijibizana na abiria tena kwa maneno makali jambo lililowashangaza abiria waliokuwa katika eneo lile.

Baadhi ya abiria wakaanza kuzungumza kwa sauti kuwa ndiyo kawaida ya wahudumu wa SGR, wengi wamekuwa hawana kauli nzuri.

Kwamba baadhi yao wanapoulizwa na abiria akihitaji maelekezo, wamekuwa hawatoi maelekezo vizuri wakidhani kila abiria anayekuwepo pale ana uzoefu na utaratibu wa usafiri.

Ni vyema sasa wakabadilika, kwani kuhudumia abiria ni wajibu wao na ndio kazi yao.

**Neema Michael,**
**Sinza, Dar es Salaam**

## Serikali itupie macho usafiri wa usiku

**Mhariri,**
NAOMBA nifikishe ushauri wangu kwa serikali kupitia gazeti lako hili tunalolipenda.

Mimi ni mpenzi wa mabasi ya abiria yanayofanya safari zake nyakati za usiku.

Tangu kuanzishwa kwa usafiri huu tumeshuhudia watu tukisafiri na kufika maeneo tunakoelekea bila shida kubwa, ingawa mwanzoni watu wengi walidhani kuwa ajali zitakuwa nyingi usiku.

Mpaka sasa ajali zimeepukwa kwa sababu madereva wengi wa mabasi yanayosafiri usiku wanakuwa makini sana barabarani. Lakini uzoefu wangu umenionyesha kuwa baadhi ya madereva wanaonekana kuanza kuzoea kusafiri usiku kiasi cha kuona kusafiri muda huo ni kawaida, hivyo, wameanza kupunguza umakini.

Kama serikali isipofanya haraka kulitazama suala hili, tunaelekea kupata madhara makubwa sana kupitia mabasi yanayosafiri usiku.

Naiomba serikali ichukue hatua ya kukaza udhibiti wa mwendo kasi wa mabasi yanayosafiri usiku ili kuondoa uwezekano wa ajali zinazoepukika.

**Hashimu Mashaka, Kihonda, Morogoro.**

## BoT idhibiti wanaotumia fedha kama shada

**Mhariri,**
KWA muda mrefu mimi ni miongoni mwa watu wanaokerwa na baadhi ya watu kufunga fedha kama shada la maua kwa ajili ya zawadi kwa wapendwa wao.

Nimefarijika zaidi baada ya wiki iliyopita Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba, kuwaonya wananchi wanaofanya hivyo, akisema kitendo hicho ni kukiuka sheria na kinachangia uharibifu wa noti za taifa.

Akasema fedha ni tunu ya taifa inayopaswa kutunzwa, hivyo inavyotumiwa kiholela huchakaa na kuchanika mapema.

Kwamba hatua hiyo ya uharibifu hulazimisha BoT kuchapisha fedha mpya mara kwa mara, jambo ambalo linaongeza gharama kwa taifa.

Binafsi naipongeza BoT kwa uamuzi huo na sasa waufanyie kazi ipasavyo, ikiwezekana wanaobainika wakifanya hivyo wachukuliwe hatua za kisheria ili kutoa funzo kwa wengine.

**Frank Kindole,**
**Mwangata,**
**Iringa.**

Kilinge cha Mawasiliano



Na Loth MAKUZA

# Kwa nini 'startups' za Afrika zitaanguka bila PR

SIKU moja niliketi pamoja na mwanzilishi wa kampuni moja changa (startup) ya teknolojia, lakini yenye matumaini makubwa.

Mwanzilishi huyo, akiwa kijana mwenye akili na ndoto, lakini pia alionekana "amechoka mno."

Akaniuliza swali rahisi; "tunawezaje kujulikana?" Nilitabasamu. Jibu langu linaonekana rahisi, lakini siyo rahisi.

Afrika, hasa Tanzania, startups nyingi zinaamini Uhusiano na Umma (PR) ni kwa ajili ya kampuni kubwa na zenye fedha nyingi. Huo ni uongo tunaoziambia nafsi zetu ili tujihisi salama.

Ieleweke kuwa startup siyo toleo dogo la kampuni kubwa. Ni cheche katikati ya kukua.

Na cheche isipolindwa, huzimika kabla hata haijaonekana. Kwa startup, PR siyo mapambo.

Ni suala la kuishi au kufa. Kujulikana siyo hiari

changamoto ya kwanza ni moja tu; umakini.

Startup haina mabavu ya kupiga kelele gizani. Haina bajeti ya mamilioni kwa ajili ya matangazo.

Ukuaji wa startup unaweza kutiwa doa kabla kampuni haijaanza kazi zake rasmi, endapo waanzislishi wake wanabeba woga.

Hapo ndipo umuhimu wa PR unapopata nafasi.

Usimulizi wa kimkakati, uzungumzwaji sahihi kwenye vyombo vya habari, na ujumbe unaotolewa kwa wakati, hujenga mwanga bila kumaliza kibubu au akiba benki.

Gazeti linaloheshimika likikuandika, jarida la sekta likikutaja, basi kazi ya PR inakuwa imetendeka.

Ujumbe unaotumwa ni mmoja; kwamba sasa wawekezaji wanaona, wateja wanaona.

Ghafla, haujulikani tena kuwa kampuni changa.

Ieleweke kuwa watu hawanunui bidhaa, wananunua imani waliyonayo kwako.

Wananunua imani kwamba wanachokipata ni salama, kizuri na kinawafaa.

Huo ndio uchawi wa Uhusiano na Umma (PR).

Tofauti na matangazo ambayo wengi huyapuuza au kuyaona kama kujisifia, PR hutegemea kufanya bidhaa ama huduma yako kuaminika.

Utafiti wa AirPR unaonyesha kuwa uwezo wa kuwageuza watu kuwa wateja kupitia PR unaweza kuwa mara 10 hadi 50 zaidi ya matangazo ya kawaida.

Wawekezaji wakiona startup yako inazungumziwa mara kwa mara inafanya kuaminika, kupata ufadhili kuwa rahisi zaidi na biashara kukua.

Soko likianza kukusikiliza, wateja wapya, masoko mapya, na fursa mpya huzaliwa.

Ukifanya hivi kwa uthabiti, washindani hufifia.

**Ushirikiano hujengwa.**

Ukikwepa PR, utabaki nyuma na hutaonekana. Mbaya zaidi, utakuwa hauhusiki na inapotokea washindani wako wakatumia PR zaidi, basi wewe unafichwa.

**PR si anasa, ni uhai.**

Startups za Afrika zitaanguka bila PR, unaweza kuwa na teknolojia bora, timu ya watendaji wenye akili, lakini kama hakuna anayejua au anayekuamini, hutakua.

Kama alivyonukuliwa Matias Rodsevich, Mkurugenzi Mtendaji wa PRLab, anasema; "PR hujenga uaminifu, huanzisha uhalali, na hufungua mawasiliano na hadhira muhimu. Ni zaidi ya kutambulika, simulizi yenye nguvu huchochea ukuaji, hupata wawekezaji, na huandaa mafanikio ya muda mrefu."

Sasa basi, kwa mwanga huo, ni dhahiri kuwa PR siyo anasa, siyo bajeti ya ziada, na siyo kitu cha "tutafanya baadae."

Chaguo ni lako.

***Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz***



Na Rashid MTAGALUKA

# Watendaji serikalini wazingatie kauli ya Mtanda



KAULI ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda (pichani), aliyoitoa Ilemela wiki iliyopita wakati wa ukaguzi wa ujenzi wa maabara ya Shule ya Sekondari Masemele, kwamba viongozi wasisubiri mitandao ya kijamii kuibua changamoto za shule kabla ya kuchukua hatua, imegusa tatizo la muda mrefu katika utumishi wa umma.

Kwa zaidi ya miaka kumi sasa, mitandao ya kijamii imekuwa kama kengele ya tahadhari kwa serikali.

Picha za wanafunzi waliokaa chini kwa kukosa madawati, madarasa yenye nyufa na upungufu wa vyoo kusambaa kwa kasi, na ghafla viongozi huonekana wakifika eneo la tukio kutoa maagizo.

"Ni aibu kubwa kwa wanafunzi kukaa chini halafu picha zimesambazwa mitandaoni ndipo tuanze kukimbizana kutafuta suluhu. Tusifike huko", alikaririwa akisema Mtanda.

Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika miaka tofauti zimewahi kubainisha upungufu wa madarasa, madawati na vyoo katika baadhi ya halmashauri. Hizi ni changamoto zinazojulikana kwenye mifumo rasmi.

Lakini hoja ya Mtanda inapopata uzito ni katika zile changamoto nyingine. Anachosema siyo tu kuhusu kukagua madawati au matundu ya vyoo, anazungumzia falsafa ya uongozi wa karibu.

Kwamba kiongozi anatoka ofisini, anaenda shuleni, anaingia darasani, anauliza maswali, anaona kwa macho yake.

Katika mfumo wetu wa utawala, halmashauri ndizo zenye jukumu la moja kwa moja kusimamia shule za umma. Zinaposhindwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara, pengo hilo hujazwa na wananchi kupitia mitandao. Lakini mitandao si chombo cha usimamizi wa serikali. Ni kioo tu cha kasoro zilizopuuzwa.

Tanzania imekuwa ikiwekeza fedha nyingi katika elimu kupitia mipango kama EP4R, BOOST na miradi ya ujenzi wa madarasa kupitia fedha za UVIKO-19. Lakini uwekezaji haukamiliki bila ufuatiliaji. Ukaguzi wa mara kwa mara ndio unaohakikisha fedha za umma zinageuka matokeo halisi.

Katika baadhi ya maeneo, ziara za kushtukiza za viongozi ziliibua madarasa yasiyotumika ipasavyo au miradi iliyocheleweshwa bila sababu za msingi. Hii inaonesha kuwa changamoto zipo, ila zinahitaji macho ya uongozi makini.

Rais Samia Suluhu Hassan amesisitiza uwajibikaji na ubora wa huduma kwa wananchi. Lakini maono ya juu hayawezi kutimia kama ngazi za chini hazichukui hatua kwa wakati.

Kauli ya Mtanda ni ukumbusho kwamba uongozi haupimwi kwa uwezo wa kujibu lawama mtandaoni, bali kwa uwezo wa kuzuia lawama zisitokee.

Katika zama hizi za kidijitali, presha ya mitandao ni kubwa. Lakini kiongozi bora hapaswi kuongozwa na presha, bali na dhamira. Mtoto anayekaa chini darasani si picha ya kusambazwa mtandaoni; ni ndoto ya taifa inayotakiwa kulindwa.

Hoja hapa ni kwamba, hili si suala la Mwanza pekee. Ni funzo la kitaifa. Tukikubali kuwa mitandao iwe chanzo cha uwajibikaji, tutakuwa tumekubali kushindwa kwa mifumo yetu. Lakini tukirudisha ukaguzi na ufuatiliaji kuwa utamaduni wa kazi kama alivyoshauri Mtanda, tutakuwa tumejenga misingi imara ya uongozi wa kweli.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***

Mazingira

# Wataalamu wakerwa ujenzi wa hoteli ndani ya Msitu wa Ngezi


*Sehemu ya Msitu wa Ngezi ambazo sasa inawekwa uzio. (Picha na Mpigapicha Wetu)*

**Na Mwandishi WETU, Pemba**

UJENZI wa hoteli ya kitalii ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Ngezi uliopo kisiwani Pemba, umeanza kuwa kero baada ya wamiliki kufunga njia iliyozoeleka kutumiwa na wananchi pamoja na maofisa hifadhi.

Wamiliki wa hoteli hiyo sasa wameweka msingi wa uzio, huku wakifunga mabati baadhi ya sehemu kuzinga njia iliyozoeleka kwa wananchi. Ujenzi huo ulianza Desemba mwaka jana – 2025.

Uzio huo wa mabati unafunga njia ambayo pia maofisa misitu na hifadhi wanatumia katika shughuli zao.

Katika ripoti yake kwenda kwa Mdhamini Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, huku nakala ikipelekwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa Misitu Zanzibar ya Desemba 18, 2025, Ofisa Mfawidhi Mkuu wa Misitu Pemba amesema ujenzi wa Hoteli ya Mantuli ndani ya Msitu wa Hifadhi wa Ngezi-Vumawimbi haujafuata taratibu za wizara na kushauri yafanyike marekebisho haraka.

Ujenzi huo unaofanywa na Kampuni ya Wipi kutoka China, pia unadaiwa kuhatalisha shughuli za kitalii ndani ya msitu huo kwani njia ya kwenda katika eneo maarufu la kuendeleza utalii nayo imefungwa, hivyo kuwalazimu hata maofisa wake na wale wa hifadhi kuzunguka ili kufika maeneo yao ya kazi.

"Nawasilisha barua hii nikiambatanisha na ripoti ya hali ya msitu hivi sasa kwa ajili ya hatua zako," ilieleza sehemu ya ripoti iliyowasilishwa kwa "wakubwa." Ripoti hiyo pia imebainisha kwamba shamba la miti ya kutengeneza mipira au maarufu plastiki (rubber farm) limeathirika.

Anasema ofisi yake haina taarifa za ujenzi wa hoteli hiyo ya hadhi ya nyota tano ndani ya hifadhi na kwamba ofisi yake na wananchi wa Konde wanajaribu kumtafuta mwekezaji au wawakilishi wake bila mafanikio.

"Tulipowasiliana na msimamizi wa ujenzi katika eneo hilo alisema mwekezaji amepewa eneo zima lililozungushiwa uzio kwa ajili ya ujenzi na Mamlaka ya Kuendeleza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA).

Wanaharakati wa mazingira, watafiti na baadhi ya wananchi wa Konde wanapinga ujenzi wa hoteli hiyo ndani ya hifadhi wakisema utaathiri miti na mimea ya asili na kuathiri shughuli za utalii ndani ya hifadhi hiyo.

Inaendelea Uk. 27

# Wataalamu...

Inaendelea Uk. 26

Msitu huo mkubwa wa pekee katika Kisiwa cha Pemba - wenye miti yenye umri mkubwa ikiwamo yenye zaidi ya miaka mia, umekuwa kivutio kikubwa cha utalii wa asili kwani ndani yake pia kuna mapango na sehemu za maalumu za kufanyia matambiko ya kimila.

"Tunaunga mkono uwekezaji katika hifadhi, ila tunashauri kwamba uwekezaji huo ni lazima ufuate taratibu na miongozo ya wizara," alisema ofisa huyo katika ripoti yake akisisitiza kwamba uamuzi wa ZIPA ni mzuri ila mwekezaji huyo anakiuka taratibu.

Amependekeza kwamba ujenzi wa uzio katika eneo kubwa la hifadhi unaoziba njia ni kukiuka taratibu na miongozo ya wizara na kushauri jambo hilo lilekebishwe mara moja ili kuwezesha wananchi kuendelea na shughuli zao za utalii bila bughudha.


Mkurugenzi wa ZIPA, Saleh Saad Mohammed na Mwakilishi waJjimbo la Konde, Zawadi Amour Nassor wanatetea ujenzi wa hoteli hiyo wakisema ni mpango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendeleza miundombinu ya utalii katika Kisiwa cha Pemba.

"Serikali ya Zanzibar imeamua kuendeleza miundombinu ya kitalii kisiwani Pemba ili kuongeza idadi ya watalii wanakuja kutembelea visiwa hivi ili kuboresha kipato na maisha ya wananchi," alisema Mohammed wakati wa kongamano la kuendeleza utalii kisiwani Pemba mwishoni mwa mwaka jana.

Mkurugenzi huyo wa ZIPA amesema pamoja na uwepo wa fukwe bora na hifadhi za asili kama Msitu wa Ngezi, Pemba imekuwa ikipata watalii wasiozidi elfu 50 kwa mwaka ukilinganisha na zaidi ya milioni moja wanafika Unguja kwa sababu ya miundombinu hafifu.

Mwakilishi wa Konde, Nassor aliunga mkono hoja hiyo akisema alifanya mikutano ya hadhara na wananchi wa jimbo hilo kuelezea mradi huo ambao utaongeza kipato cha wakazi wa kisiwa hicho cha pili kwa ukubwa katika visiwa vya Zanzibar.

"Serikali inajenga barabara, viwanja vya ndege kama sehemu ya kuboresha miundombinu katika visiwa vya Pemba kwa manufaa ya watu wote na wawekezaji wanakuja kutuunga mkono," alisema mwakilishi huyo.




*Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi*

Watafiti wa mimea na uota wa asili kutoka vyuo vikuu kadhaa vya Tanzania, Kenya, Uingereza, Italia na Marekani, hivi karibuni walichapisha barua ya wazi katika Jarida la Sayansi la Chuo Kikuu cha California - Kampasi ya Davis wakionya kuhusu ujenzi wa hoteli hiyo ambao wanadai utaathiri asilimia 23 ya hifadhi.

"Ili kulinda eneo la hifadhi la pekee kisiwani Pemba, tunashauri mamlaka za Zanzibar kusitisha ujenzi wa Hoteli ya Mantuli Luxury Resort na kupeleka mradi huo eneo tofauti na hifadhi," walisema watafiti hao wakiongozwa na Profesa Tim Caro kutoka Chuo Kikuu cha Bristol nchini Uingereza.

Katika barua hiyo iliyochapishwa Septemba mwaka jana 2025, watafiti hao walitahadhalisha kwamba uwekezaji wa dola million nane (zaidi ya Shilingi bilioni 17.3) utaathiri mimea ya pekee ndani ya hifadhi pamoja na miti yenye umri wa zaidi ya miaka 100 ambayo ni muhimu kwa visiwa vya Zanzibar ambavyo vinatishiwa na mabadiliko ya tabia nchi.





Na Anti MSHAURI

# Wanandoa zingatieni haya kudumisha uhusiano



HABARI za leo msomaji wangu wa safu ya Uhusiano.

Karibu uonje ladha ya uhusiano mzuri kupitia mada mbalimbali zinazokujia kila wiki.

Wiki hii nitazungumzia mambo ya kuzingatia kwa wanandoa na walio kwenye uhusiano kama njia ya kudumisha ukaribu wao.

Uhusiano mzuri unahitaji kazi na kujitolea kwa hali na mali. Kutokana na uhusiano wa wengi kuzidi kuporomoka siku hadi siku kutokana na changamoto mbalimbali na ili kufanikisha hayo wanandoa wanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo;

Wasiliana kwa ufanisi; mawasiliano ni msingi wa uhusiano mzuri. Jifunze kusikiliza kwa makini na kuelezea hisia zako kwa uwazi.

Shukuru na kujali; unapaswa kuonyesha shukrani na kujali kwa mwenzako kila siku. Hii inaweza kuwa kwa maneno, matendo, au zawadi mbalimbali.

Fanyeni mambo pamoja; kila mmoja anapaswa kupata muda wa kufanya mambo pamoja na mwenzake, hata kama ni kitu kidogo kama kutazama filamu, kupika pamoja na mengine.

Kusamehe na kusahau; katika hilo wana uhusiano mnapaswa kusameheana na kusahau makosa yote mliyofanyiana kwani hakuna uhusiano usio na changamoto ingawa zinatofautiana.

Wekeaneni kipaumbele ili muweze kufanya mambo yenu ya maisha kwa mpangilio; Hapa mnaweza kutenga mambo ya kufanya kwa mwaka mzima mfano kujenga, kulipa ada za watoto na mengine.

Panga muda wa kuwa pamoja na kufanya mambo unayoyapenda; Hapa mnaweza kutenga muda wenu na kuamua kwenda kupumzika nje ya nyumbani mfano hotelini, ufukweni na maeneo mengine yatakayowafanya muwe na furaha.

Mkizingatia haya, wanandoa na mlio kwenye uhusiano mtayafurahia maisha yenu kwa kiasi kikubwa.

Tukutane wiki ijayo.

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***



# Nguo zitakazokufanya uonekane mrefu

BINADAMU tumeumbwa kwa kila mmoja kupewa kimo chake, hatulingani; wapo warefu na wafupi pia.

Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya fasheni, unaweza kuvaa ukajiongeza urefu kupitia nguo na viatu.

Hapa chini nimekuwekea dondoo za kukuwezesha kupata muonekano uutakao;

Kama wewe ni mfupi, pendelea kuvaa magauni. Hii itakusaidia kwa kuwa ni nguo moja hadi chini haijajigawa kama sketi na blauzi hivyo inakuza kimo chako.

Nguo za mistari, niliwahi kuandika hili kuwa nguo za mistari iliyosimama inakufanya uonekane mrefu na kuwa mwembamba kiasi fulani tofauti na mistari iliyolala ambayo inakufanya mnene zaidi.

Bwanga; hili nalo ni moja ya vazi bora kwa mtu mfupi, vaa pamoja na topu ndogo/chomekea au vaa crop top na viatu vya kufunika virefu.

Jitahidi 'kumechisha' top na viatu kwani itakusaidia kuufanya muonekano wako uwe wa kuvutia zaidi.



# Tunza nywele asili hivi

Osha nywele zako vizuri kwa kutumia shampoo ambayo imetengenezwa maalumu kwa nywele asili au iliyotengenezwa kwa ajili ya nywele zenye dawa ambayo ina conditioner.

Tumia mafuta ya kama vile ya nazi, olive oil, jojoba oil au castor oil kwa sababu mafuta haya hulainisha ngozi ya kichwa, kufanya nywele zikue vizuri na kuzuia mba.

Usiache kuzifanyia steaming nywele zako kwa mwezi hata mara moja huku ukizichana vizuri nywele zako kwa mafungu na kufunga makonga.





# Britney Spears auza nyimbo kwa dola milioni 200

Na Mwandishi WETU

MWANAMUZIKI wa Pop na mwigizaji kutoka Marekani, Britney Spears, ameripotiwa kuuza haki za katalogi yake yote ya muziki katika mkataba unaokadiriwa kufikia dola za Marekani milioni 200.

Britney, mwenye umri wa miaka 44, inadaiwa kuwa amekamilisha makubaliano yote Desemba 30, 2025 na kampuni huru ya muziki Primary Wave. Hata hivyo, thamani halisi ya mkataba huo haijatangazwa rasmi.

Mwanamuziki huyo ni mmoja wa wasanii wa kike waliouza nakala nyingi zaidi duniani.

Britney alianza kupata umaarufu wa kimataifa mwishoni mwa miaka ya 1990.

Tangu alipoanza muziki, mwaka 1999 alitoa albamu tisa za studio na kuuza zaidi ya nakala milioni 150 duniani kote. Pia ameshinda tuzo mbalimbali ikiwemo Grammy.

Mwaka 2024, alitangaza kuwa hatarudi tena katika tasnia ya muziki.

# Baba Levo: Walioshindana na Diamond walifilisika

Na Mwandishi WETU

MBUNGE wa Kigoma Mjini, Clayton Revocatus almaarufu Baba Levo, amemfagilia Diamond Platnumz baada ya kutoa video ya wimbo mpya wa "Natulizana."

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Baba Levo alipost video ya wimbo huo huku akimsifia Diamond uwekezaji anaoufanya kwenye muziki wake, akiwataka wasanii wengine wasishindane na msanii huyo nguli na kwamba walioshindana naye walifilisika.

"Huyu Diamond ni tunu kubwa sana kwenye nchi yetu… anaweza kukaa kwenye nafasi ya kwanza kwenye jukwaa la muziki wa Tanzania kwa zaidi ya miaka 16.

"Nimetumia muda mwingi sana kuwaelimisha wasanii wa bongo fleva, wasishindane na Diamond ila waungane naye kusogeza gurudumu la muziki wa Tanzania kimataifa," aliandika Baba Levo.



# Jinsi ya kusoma Pambazuko


rifaly

## Soma Gazeti la Pambazuko Popote Ulipo!




Scan QR Code Kusoma

**Jinsi ya Kusoma Pambazuko Ndani ya Rifaly**

- **Scan QR Code** – Itakupeleka moja kwa moja kwenye channel ya Pambazuko ndani ya **Rifaly.**
- **Jisajili au Ingia (Log In)** – Tumia namba ya simu, barua pepe, au akaunti ya Google.

Furahia Kusoma Pambazuko muda wowote na mahali popote ulipo.

Pakua Rifaly Sasa na Anza Kusoma



# Haya yafanyike kuipa Tanzania ubora Afcon 2027



Beki wa Taifa Stars, Dickson Job

Na Mwandishi WETU

KUWEPO kwa taarifa za kupanda kwa kiwango cha soka la Tanzania katika jedwali la FIFA ni dalili nzuri, lakini kudumu kwake hadi wakati na baada ya michuano ya Afcon 2027 kutategemea mchanganyiko wa sababu za kiufundi, kifedha na kiutawala.

Kwanza, utendakazi wa timu kitaifa wakati wa mechi za kwanza za kufuzu na mechi za kirafiki za kimataifa, utaamua kiasi cha alama zitakazoongezeka kabla ya Afcon ijayo.

Mechi na wapinzani wake. Timu za mataifa mengine, zenye viwango vya juu hupandisha viwango zaidi ikitokea Tanzania inapata matokeo mazuri; hivyo ratiba ya mechi za kirafiki za kimataifa ni muhimu zaidi kwa sasa.

Pili, utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya wachezaji chipukizi na kuimarisha Ligi Kuu ya Tanzania ni muhimu. Ikiwa vilabu vitaendelea kuwekeza katika vijana, utunzaji wa wachezaji na kocha bora, basi mtiririko wa talanta utaendelea, ukitoa faida endelevu kwa timu ya taifa.

Mafunzo ya kitaalam kwa makocha na mfumo wa utambuzi wa wachezaji wa diaspora unaweza kuongeza wigo wa talanta.

Tatu, usimamizi wa serikali kwa timu ya taifa – Taifa Stars, kupitia Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) ni jukumu kuu ambalo sasa wizara inatakiwa kusimamia kwa ukaribu zaidi.

Pia kuwepo kwa motisha kwa wachezaji, benchi la ufundi na uwazi katika fedha, utekelezaji wa sera za kitaaluma, na malipo ya haki kwa makocha/ wachezaji ni njia nyingine bora kuongeza morali na utulivu.

Uwekezaji wa miundombinu, hasa vituo vya mafunzo na uboreshaji wa viwanja, nako kutachochea matokeo mazuri kwa Taifa Stars kwa michezo ya ndani na kimataifa.

Nne, masuala yasiyotegemewa kama majeruhi, adhabu za FIFA, au matatizo ya kisiasa yanaweza kupunguza kasi ya kupanda kwa kiwango cha Tanzania, hivyo umakini wa serikali na viongozi wa siasa unahitajika zaidi.

Kwa upande mwingine, mafanikio katika Afcon 2027, yanaweza kuipandisha zaidi Tanzania katika viwango vya FIFA na kuwa fursa muhimu kwa wachezaji wa ndani kupata kandarasi kubwa nje ya Afrika.

Aidha, matokeo ya muda mfupi yatategemea ratiba na utayari wa serikali kuhudumia Tafa Stars, lakini kudumu kunahitaji sera za muda mrefu, uwekezaji katika vijana, makocha wazuri, usimamizi imara, na mechi za kimkakati ili “kuipa joto” Taifa Stars.

Ikiwa haya yatatekelezwa, Tanzania ina nafasi kubwa ya kufanya vyema katika michuano ijayo ya Afcon ambayo itafanyika kwa mtungo wa nchi tatu za Afrika Mashariki; Tanzania, Kenya na Uganda.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION